SUPA JACKPOT
TZS. 1,114,965,687
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**RC** ashtukia jambo vigogo halmashauri waliosimamishwa kwa tuhuma ufisadi wa milioni 380/-

UKURASA 7



**KLOPP: LIVER ITAPIGANIA NNE BORA HADI MWISHO**

UKURASA 21

Nipashe
Jumatano Mei 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581313
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# KISHINDO CHA ELIMU

- **Ufadhili** wa Samia wapaishwa, vinara kusoma bure vyuo vikuu, ufundi wafufuliwa kisasa...

*Endelea ukurasa 2,9,10,11,12 & 13*

- Waajiri 8,000 kugongewa hodi na HESLB
- Mabilioni yaandaliwa mikopo elimu ya juu
- Kila wilaya nchini sasa kuwa na VETA
- Vyuo vya Walimu kuboreshwa
- Kozi kwa walimu maelfu Hisabati, Sayansi, KKK



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kariakoo bado msimamo ule ule, mgomo siku ya 2

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mkewe, Mary wakiweka shada la maua kwenye kaburi la Bernard Membe, alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika maziko yaliyofanyika kijijini Rondo mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

## Hivi hapa vigingi 10 kwa Chalamila Dar

UK.4

MICHEZO · YANGA YAPANIA HISTORIA SAUZI LEO UK.24 · KATUNI UK.6




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Arusha jana, wakati akiwakaribisha wanahisa wa benki hiyo katika Mkutano Mkuu wa 28 utakaofanyika Jumamosi Mei 20 mwaka huu. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati) na Katibu wa Kampuni wa benki hiyo, John Rugambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kishindo cha Elimu 2023/24

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, katika mwaka ujao wa fedha unaoanza Julai Mosi, imekuja na mikakati inayobeba mageuzi katika yale inayoyaendeleza, pia mapya yanayoendana na mahitaji nchini na kimataifa.

Katika wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo jana bungeni, Waziri wake, Prof. Adolf Mkenda, alitaja maeneo yanayoguswa ni mageuzi katika Tehama na mafunzo yake huku walimu wakinolewa kukidhi mahitaji ya sasa.

Vilevile, waziri alitaja fursa kwa wanafunzi bora wa kidato cha sita kunufaika na elimu ya bure vyuo vikuu. Pia ufadhili wa Rais Samia Suluhu Hassan utatanuliwa maradufu, kama itakavyokuwa kwa mikopo ya elimu ya juu.

Wizara hiyo katika wasilisho lake imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha vijana wa kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika. Imeliomba Bunge kuidhinishia Sh. trilioni 1.675 kufanikisha mikakati hiyo kwa mwaka 2023/24.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 537,881 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Sh. bilioni 501 ni mishahara na Sh. bilioni 36.923 kwa ajili ya matumizi mengineyo). Sh. trilioni 1,138 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo Sh. bilioni 979.084 fedha za ndani na Sh. bilioni 158.789 zitatolewa na washirika wa maendeleo.

Waziri Mkenda alivitaja vipaumbele vyao ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji.

Katika hilo, alisema serikali itafanya mapitio na marekebisho ya Sheria ya Elimu kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na sheria mbalimbali za Taasisi za Elimu ili ziendane na mahitaji ya toleo jipya la sera na mitaala.

Alivitaja vipaumbele vingine ni kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali (ufundi) katika elimu ya sekondari na vyuo vya kati vya amali; kuongeza fursa na ubora wa elimu ya msingi na sekondari; kuongeza fursa na ubora wa elimu ya juu; na kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Prof. Mkenda alisema wizara hiyo pia itaandaa Mwongozo wa Chakula na Lishe pamoja na Mwongozo wa Utunzaji wa Mazingira katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa lengo la kuhakikisha viwango vya utolewaji wa chakula katika vyuo vinatekelezwa ipasavyo na watoa huduma.

"Pia tutakarabati shule za sekondari za ufundi na kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuboresha vyuo vya ualimu 10 ikiwa ni pamoja na Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi na kuwawezesha walimu tarajali kupata mafunzo ya Shahada ya Amali kwa kutumia wahitimu wa Vyuo vya Ufundi (TET) na Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET).

"Wizara itajenga karakana 10 na kuweka mitambo na vifaa katika vyuo vya ualimu ambavyo ni: Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara (U), Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga kwa lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi kwa vitendo," alisema.



Pia alisema wizara hiyo itahakiki udahili wa wanafunzi 250,000 wa vyuo hivyo, kuongeza idadi ya walimu wa amali katika taasisi za umma kutoka 788 hadi 900. Kutoa mafunzo kwa walimu 1,300 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri (CBET).

Waziri huyo pia alisema watajenga vyuo vya ufundi katika wilaya 64 ambazo hazina vyuo hivyo; kununua magari 12 kwa ajiri ya wathibi ubora wa elimu na kuziwekea samani ofisi 195 za kada hiyo; watatoa mafunzo kwa walimu maelfu wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi.

Prof. Mkenda pia alisema wizara ya itaboresha miundombinu ya shule za sekondari za ufundi; kupanua hosteli za Magufuli na kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka 202,877 mwaka huu hadi 210,169 mwaka ujao wa fedha.

Pia alisema watapanua ufadhili wa Samia kutoka wanufaika 593 mwaka huu hadi 1,200 mwaka ujao huku vinara wa ufaulu 70 wakifadhiliwa kusoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM - wanafunzi 50) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM - wanafunzi 20).

Prof. Mkenda alisema katika mwaka ujao wa fedha, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) itawafikia waajiri takribani 8,000 kwa lengo la kukagua urejeshaji wa wanufaika wa mikopo inayoitoa.

*SOMA HOTUBA UK. 9-13

## Ummy asema hakuna kifo cha UVIKO-19 kilichothibitishwa

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hakuna kifo kilichothibitishwa kimesababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19, huku akiwataka wananchi kutokuwa na hofu bali wawe watulivu wakati serikali inafuatilia kwa karibu.

Waziri Ummy alibainisha hayo jana kupitia mtandao wake wa kijamii, kutokana na kuwapo kwa sintofahamu na mijadala inayoendelea kwenye mitandao ya kijami kuhusu kuibuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19, nchini.

"Kwa taarifa za wagonjwa waliopimwa virusi vya UVIKO-19 wiki ya tarehe 6 hadi 12 Mei, mwaka huu, watu sita kati ya 288 walithibitishwa kuwa na ugonjwa huo, ikiwa ni pungufu ikilinganishwa na wiki ya Aprili 29 hadi Mei 5, mwaka huu," alisema Waziri Ummy.



Aidha, ujumbe wake katika mtandao wake wa kijamii aliambatanisha picha iliyokuwa na maneno yakisomeka "Utaratibu ni ule ule tunaendelea nao, ukisubiri matangazo shauri yako".

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi kuondoa hofu wakati huu serikali ikiendelea kuchakata taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma ya afya ndani ya wiki ili kuujuza umma kuhusu hali hiyo, huku akiwaomba wananchi kuendelea kuzingatia kanuni za afya na usafi.

Mwananchi aliyejulikana kwa jina la @husnmann, aliandika kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram akisema "COVID haikuwahi kuisha ila imepungua na tunaishi nayo kama magonjwa mengine ya kuambukiza.

"Sijui kwa nini serikali inakigugumizi kwenye hili, tunaofanya kazi hospitali tunajua hivyo, 'issue' (jambo) sio kuwatisha watu ila ni kuwafanya wachukue tahadhari," alisema.

Naye @aminadesign alisema aliumwa mwezi mzima na kubadili hospitali mbalimbali kubwa, lakini hakupona, na kwamba mchanganyiko wa tangawizi, vitunguu maji na swaumu, limao, pilipili, asali na manjano ndivyo vilivyomsaidia na ndani ya siku tatu alipona.

Vile vile, @mariamu6157 aliandika: "Kikubwa tuchukue tahadhari ni kama vile malaria inaua ukizembea, pia Ukimwi na kifua kikuu, kama tumeshaelewa kuingia ugonjwa ni rahisi, lakini kuondoka kabisa inachukua muda, tunaamini Watanzania tunajielewa, tutazingatia usafi kwa usalama zaidi."

# Mgomo Kariakoo msimamo ule ule

**Na Halfani Chusi**

MGOMO wa wafanyabiashara Kariakoo, jijini Dar es Salaam, umeingia siku ya pili huku baadhi wakisema wanasubiri kikao kitakachofanyika leo kati ya viongozi wao na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa ajili ya kutatua kero walizoziainisha kwa muda mrefu.

Waziri Mkuu Majaliwa, juzi majira ya jioni alikatisha shughuli za bunge Dodoma na kufika kwenye soko hilo kusikiliza kero zao kujaribu kuzitatua, huku akiwaahidi kujadili kwa kina na viongozi wa wafanyakazi hao mustakabali wa sakata hilo leo.

Hata hivyo, kauli hiyo haijawa suluhu baada ya jana wafanyabiashara hao kuendelea na mgomo huo, huku wengine wakiendelea kufunga maduka yao na wengine kushikilia msimamo huo.

Jana, Nipashe ilitembelea mitaa mbalimbali ambayo wafanyabiashara walionekana wamekaa nje ya maduka, huku kwenye makundi songezi wakiendelea kuhamasishana kutofungua maduka hadi serikali itakapotatua kero zao.

Mfanyabiashara wa vifaa vya magari na pikipiki katika Mtaa Sikukuu, Samson Juma, alisema wanaendelea na mgomo huo kwa sababu Waziri Mkuu hakujibu hoja zao ipasavyo ndiyo maana wameendelea na msimamo wa awali.

“Waziri Mkuu kweli ameongea vizuri na tunashukuru kwa kuchukua hatua za haraka kuja kutusikiliza lakini aliwahi kuongea kipindi cha nyuma mambo kama yale na hayakutekelezwa shida ilibaki pale pale,” alisema.

Mfanyabiashara wa duka la vipodozi, Asia Shabani, alisema wameendelea na mgomo huo kwa sababu viongozi wao wameshindwa kuwapa mrejesho mzuri wa kikao cha ndani walichofanya na Waziri Mkuu juzi.

“Viongozi wetu wa soko tuliowachagua hawafai kuwa viongozi, hawana sifa. Kweli wameongea na Waziri Mkuu juu ya sakata hili lakini hawakupaswa kutumia hasira wanapotueleza sisi wafanyabiashara,” alisema.

Jana asubuhi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mmbwana, aliwasihi wafungue biashara kwa kuwa serikali imewasikia na watakutana kwenye kikao kitakachoweka suluhisho la kudumu.

Alisema mwenyekiti aliwalazimisha wafunge biashara bila kujua hatima yake itakuwaje amefikia hatua mpaka anasema: “fungueni maduka yenu kama hamfungui mimi ninajiudhulu siwezi kuwa kiongozi wenu tena.”

“Hiyo si kauli nzuri ya kutumia kiwa kiongozi, kwa hiyo sisi tunaendelea kugoma mpaka majibu yatakayoamuliwa kesho (leo) kama hayataridhisha pia tutaendelea kugoma,”alisisitiza.

Mfanyabiashara mwingine wa bidhaa za urembo, Aisha Ali, alisema mgomo huo umewaathiri kwa kiasi kikubwa na kwamba shughuli nyingi zimekwama kutokana na kufungwa kwa maduka.

Aliiomba serikali kutatua kero zao ambazo walianza kupeleka malalamiko yao kwa njia ya kuandika barua muda mrefu bila utatuzi.

“Kauli ya Waziri Mkuu jana ilikuwa nzuri, lakini bado kuna shida, wateja kutoka nje wanaathirika kwa sababu hawapati bidhaa wanakuta maduka mengi yamefungwa, wengine wamekopa mikopo wanatakiwa kulipa madeni na wananchi wa chini ndio wanaathirika zaidi,” alisema.

Mfanyabiashara mwingine wa Mtaa wa Muhonda, Agnesi Shayo, aliwashauri wenzake kusikiliza kauli ya Waziri Mkuu, akisisitiza kuwa aliahidi kutusikiliza na kutatua kero zetu leo.

“Ninaona tuitii serikali, ikiamua kutususia hili suala sisi ndio tutapata shida, ninahisi wafanyabiashara tunauelewa tofauti, lakini ninaona Waziri Mkuu, alikuwa sahihi na ameahidi kutekeleza ombi letu siku ya leo sasa shida iko wapi?” Alihoji.

Kwenye kundi songezi, wengi wao waliotuma maoni walisema hawajaridhika na hatua za sasa hadi waone kero zao zimetatuliwa.

Sauti hiyo iliyorekodiwa na mmoja wao ilisema: “Wafanyabiashara jambo letu liko palepale...sisi jambo letu toka Jumatatu ni kufunga maduka, kuhusu mwenyekiti wetu ukiongea serikali ina mkono mrefu.

Alisema wanapaswa kumtia moyo, kwa kuwa mgomo huo sio kwa maslahi yake peke bali ni kwa wafanyabiashara wote.

“Kesho (leo) tutasikilizwa ili tupate majibu yetu, na yawe kama vile tulivyoesema yasiwe kwa maeneo yawe kwa maandishi sheria zibadilishwe na tuambiwe zimebadilishwa tusikubali tena,”alisema.

Mbwana alisema hali ilikuwa nzuri asubuhi kuanzia majira ya saa moja hadi mbili lakini baadaye kidogo ikabadilika.

Alisema, kubadilika huko kumetokana na maslahi binafsi ya watu wachache, akidai kuwa wapo wanaopata maslahi kutokana na mgomo huo.

Kuhusu wafanyabiashara kudai hawajaridhishwa na hatua za Waziri Mkuu na kwamba ameongea maneno ya kisiasa alisema: “Niliwasilisha hoja hiyo kwa Waziri Mkuu kwenye kikao cha ndani akamsimamisha kamishna wa kodi za ndani akamuuliza unataka barua iandikwe kwa nani? Unataka barua kwa nani? Kwa utaratibu upi?

“Nakatoa maelekezo kwamba tamko la Rais ni amri. Sasa nashangaa wamegoma kwamba hawana imani na Waziri Mkuu, wakati tumepaza sauti kwa Rais amemtuma mtendaji wake mkuu akatuomba tufungue maduka.”

**POLISI YAINGILIA**

Jana Kamamda wa Polisi Kanda Maalumu Dar es Salaam, Jumanne Murilo, alitembelea Kariakoo na kuonya kitendo cha baadhi ya wafanyabiashara hao kuzuia waliotii agizo la kufungua biashara zao.

“Wewe kama unafunga biashara yako funga lakini kumtisha anayefungua hilo ni kosa hapo utakuwa unatuchokoza sisi tusije tukalaumiana kwenye mchezo huo,” alionya.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.05.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe 19-05-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea **JNHPP SITE,** gari hizo zina namba za usajili: **T 622 DFA / T 416 AYQ T 641 DFA / T 321 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 5.50**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE** kupitia **KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.** Gari zitasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Usiku mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.05.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe **20-05-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea JNHPP SITE, gari hizo zina namba za usajili: **T 482 ECF / T 568 EAZ T 639 DFA / T 390 DHQ T 178 DFC / T 310 DDH T 118 EAG / T 877 EAU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 6.90**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar es Salaam Port mpaka Bungu.** Kutoka **Bungu kwenda JNHPP Site** gari zitasafiri muda wa mchana ( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.05.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **18-05-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero** kupitia Mikumi, gari hiyo ina namba ya usajili: **T 866 DDL / T 269 DUH T 903 DSD / T 380 DHQ**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 23.00**
   **Upana - mita 4.50**
   **Kimo - mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17.05.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe **20-05-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea **JNHPP SITE,** gari hizo zina namba za usajili: **T 460 DYG / T 879 EAU T 503 ECF / T 777 AQR T 973 DTN / T 572 EAZ T 490 ECF / T 881 EAU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.00**
   **Upana - mita 7.25**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM** hadi **JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar es Salaam Port mpaka Bungu. Kutoka Bungu kwenda JNHPP Site** gari zitasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilboard Mutafungwa akizungumza na waandishi na wadau wa habari kutoka Taasisi mbalimbali, katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, jijini humo jana. **PICHA: ROSE JACOB**

# Hivi hapa vigingi 10 kwa Chalamila Dar

**Restuta James na Halfani Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan juzi alifanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa minne kwa kuwahamisha vituo vya kazi.

Mabadiliko hayo yanaonekana ya kawaida na yanalenga kuimarisha utendaji kazi serikali lakini kibarua kizito kinaonekana kumwelemea zaidi Mkuu mpya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.

Chalamila kabla ya kuhamishiwa Dar es Salaam, alikuwa na wadhifa kama huo mkoani Kagera na kuingia kwake moja kwa moja anakutana na mgomo wa wafanyabiashara wa Kariakoo ambao leo unaingia siku ya tatu.

Kiongozi huo ambaye alishika wadhifa huo tangu serikali ya awamu ya tano chini ya hayati Dk. John Magufuli, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera Julai 28, mwaka jana. Kabla ya hapo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na baadaye Mwanza na kuwa nje kwa miezi kadhaa baada ya Rais Samia kutengua uteuzi wake.

Chanzo kilionekana ni kiongozi huyo kuwataka machinga kubeba mabango na kuandamana siku ambayo Rais angefanya ziara ya kikazi mkoani Mwanza. Kauli hiyo ilionekana kwenda kinyume na ile ya Rais aliyoitoa siku chache kwamba hataki kusikia malalamiko wala mabango kutoka kwa wananchi, hivyo wakuu wa mikoa na wilaya wasaidiane kutatua kero zinazowakabili wananchi badala ya kusubiri ziara ya viongozi wakuu wa serikali, Rais akiwamo.

Sifa za Chalamila zilianza kuonekana katika tukio la Aprili 28, 2021, alipowatandika viboko wanafunzi saba wa Shule ya Sekondari Iyunga mkoani Mbeya na kuwaamuru walipe kila mmoja Sh. 300,000 kwa ajili ya matengenezo kutokana na kuchoma moto chumba cha kuhifadhia vifaa vya shule.

Sasa Chalamila anaingia Dar es Salaam kuchukua nafasi ya Amos Makalla ambaye amepelekwa mkoa wa Mwanza. Kuingia Kwake Dar es Salaam, anapokewa na mgomo wa wafanyabiashara wa Kariakoo, eneo maarufu kama 'dubai ya Tanzania' kutokana na umaarufu wake kibiashara na ni kitovu cha makusanyo ya mapato ya serikali.

Mbali na mgomo wa wafanyabiashara, wachambuzi wanataja vigingi vingine vinavyomkabili kiongozi huyo mwenye mbwembwe za kila aina ni uchafu, wamachinga, mfumo mbovu wa majitaka, uhaba wa majisafi, ujenzi holela na uhaba wa madarasa pamoja na madawati. Changamoto au vigingi hivyo vinaonekana ni mtihani kwa Chalamila na anapaswa kuweka nguvu kuzitatua.

**WAMACHINGA**

Johnson Michael, mkazi wa Mbagala, aliiambia Nipashe kwamba wamachinga wamekuwa tatizo sugu kwa kuwa wanafanyabiashara kwenye masoko makubwa kama Kariakoo na vituo vya daladala kiasi kwamba wanasababisha kero kwa wateja, wapitanjia na kwenye maduka makubwa.

Alitoa mfano wa wamachinga waliopanga bidhaa pembeni ya barabara za Uhuru kwenye soko la Karume, mwisho wa kituo cha Mbagala Rangi Tatu na sokoni Kariakoo, akisema wamefunga mitaa mingi. Alisema serikali iliwahi kuwahamisha na kuwatambua wamachinga, lakini zoezi hilo halikuwa endelevu.

"Nadhani hili ni eneo atakaloliangalia sana mkuu wetu mpya," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara walio kwenye mgomo walisema wanaitaka serikali iwaondoe machinga nje ya maduka yao kwa kuwa wanachukua wateja wao huku hawalipi kodi kama wanazolipa wenye maduka.

**MAJISAFI, MAJITAKA NA TAKATAKA**

Mkazi mwingine, Atuganile Ndemwabuke, alisema Dar es Salaam inakabiliwa na mfumo mbovu wa majitaka unaochangia uchafuzi wa mazingira hususani kipindi cha mvua na chemba za majitaka hufumuka. Alisema tatizo lingine ni uhaba wa madampo jambo linalolifanya jiji liwe chafu wakati wote.

Ndemwabuke, mkazi wa Kibada, alisema kero nyingine inayomsubiri Chalamila ni uhaba wa majisafi akieleza sehemu kubwa ya jiji haijafikiwa na huduma hiyo muhimu.

Hivi karibuni, Makalla alisema dampo la Pugu Kinyamwezi limejaa hali inayokwamisha uondoaji wa takataka kwenye mitaa, huku magari yakishindwa kuzoa takataka kwa kuwa hakuna pa kwenda kuzitupa.

**UJENZI HOLELA**

Mkazi mwingine, Juliana Haule, alisema kero nyingine ni ujenzi holela hasa maeneo ya mabondeni ambayo yanamilikishwa kwa wananchi kinyume cha utaratibu.

Ikungasya Asimbile naye alisema pamoja na kwamba Dar es Salaam pia inakabiliwa na uhaba mkubwa wa madarasa na madawati, hivyo ni kipimo kingine kwa Chalamila.

"Watoto wanakaa chini wakiwa wamesongamana kiasi kwamba hawawezi kupata kile kinachotarajiwa. Mfano Kata ya Toangoma karibu shule zote watoto wanakaa chini," alisema.

**PANYA ROAD**

Kibarua kingine kikubwa ni ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kutokana na kuibuka kwa vikundi vya vijana vinavyopora na kujeruhi watu huku matukio ya ujambazi yakianza kurejea kwa kasi.

Kutokana na nafasi yake kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Chalamila ana kibarua kizito cha kukomesha tatizo hilo.

**WALIOHAMISHWA**

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu iliyotolewa juzi, mbali na Chalamila na Makalla, wengine waliohamishwa ni Adam Malima anayetoka Mwanza kwenda Morogoro na Fatma Mwassa akipelekwa Kagera kuchukua nafasi ya Chalamila.

# Sarakasi za Chalinze Cement na BRELA zafika mahakamani

**Na Kulwa Mzee**

KAMPUNI ya Saruji Chalinze imeeleza kushtushwa kuondolewa usajili bila taarifa, hivyo kufungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania kuomba imwamuru Msajili wa Kampuni chini ya Wakala wa Usajili wa Leseni na Majina ya Biashara (BRELA) kuirejesha katika daftari la usajili.

Katika hati ya kiapo iliyoandaliwa na kampuni ya mawakili ya Law Associates, waombaji hao pia wanaomba mahakama itoe amri nyingine ambayo itaona inafaa ili kuhakikisha haki ya msingi inatendeka.

Maombi hayo yaliwasilishwa mwishoni mwa wiki na waombaji wawili, Chalinze Cement Company Ltd na Mohammed Bahadela ambaye ni mwanahisa na mkurugenzi wa kampuni hiyo.

Katika maombi yao wanadai kwamba kampuni ilikuwa ikiendesha shughuli zake, inafanya biashara kwa kufuata taratibu na sheria. Inadaiwa walishtuka Aprili 25, mwaka huu, kuona katika gazeti moja ikiwa imeandika kwamba mwombaji namba moja ameondolewa katika daftari la usajili wa kampuni.

Waombaji wanadai taarifa hiyo iliwashtua baada ya kuona iko katika Gazeti la Serikali la Machi 3, mwaka huu.

Inadaiwa katika gazeti iliandikwa kwamba kampuni hiyo ilifutwa kwenye usajili kwa sababu ya kuwapo kwa taarifa za uongo wakati inaingizwa katika usajili.

"Hakuna taarifa, notisi wala mawasiliano kwa waombaji kuhusu kuondolewa kwenye usajili, taarifa hizo zilishtua. Hatukubaliani na uamuzi huo wa kuondolewa kwenye usajili bila taarifa na tumenyimwa haki ya kusikilizwa," ilidai sehemu ya maombi.

Waombaji wanadai kuwa kampuni ya Chalinze ilianzishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria kwa nia ya kukuza uwekezaji wa biashara mchakato ambao walipanga kufanya kabla mwombaji wa kwanza hajaondolewa usajili.

Kwa mujibu wa hati hiyo, waombaji walidai kuwa walihuzunishwa na kushtushwa na uamuzi wa BRELA wa kuwafuta katika usajili bila kupewa taarifa wala nafasi ya kusikilizwa, ambayo ni haki ya msingi, kabla ya kufikiwa kwa hatua hiyo.

Waombaji wanadai lengo la kufungua maombi hayo ni mahakama kumwamuru Msajili wa Kampuni kumrejesha kwenye usajili mwombaji wa kwanza, ili aendelee kuendesha biashara na mambo mengine yanayolenga kukuza uwekezaji wa biashara, biashara na maendeleo.

Chalinze Cement inahusishwa katika wadaawa wanaopinga muunganiko wa kampuni za saruji za Twiga na Tanga. Tume ya Ushindani (FCC) ilitangaza muunganiko huo kupitia Scancem International DA ambayo ni kampuni tanzu ya Heildeberg Cement inayomiliki Twiga Cement na AfriSam Mauritius Investment Holding Limited inayomiliki Tanga Cement.

Kupitia Muunganiko huo, ilidaiwa kuwa Twiga Cement angekuwa na asilimia 68.33 hali ambayo ingesababisha ukiritimba katika soko na hata kuleta athari za upatikanaji wa bidhaa na za kiuchumi kwa jumla.

Hatua huyo ilisababisha Chalinze na wadau wengine, kikiwamo Chama cha Kutetea Watrumiaji Bidhaa na Huduma (TCAS) kufungua shauri la kisheria kupinga muunganiko huo na hatimaye Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT) katika uamuzi wake wa Septemba 23, 2022 lilibatilisha mchakato huo.

# Airtel yaja na kampeni mpya kwa wateja wao

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Afrika imezindua kaulimbiu mpya ya 'A Reason to Imagine' inayolenga kujenga ujumuishi kwa wateja wa rika zote katika nchi 14 inazofanya biashara.

Akizungumzia kaulimbiu hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel, Dinesh Balsingn, alisema jana kuwa kampuni hiyo baada ya kutamba na kaulimbiu ya 'The Smartphone Network', sasa inakuja na 'A Reason to Image' kwa lengo la kuendeleza dhamira ya kuwawezesha wateja wa rika zote kufikia ndoto na matarajio yao.

Balsingn alisema "…kila mtu anayo sababu ya kufanikiwa kupitia maono, vipaji, watu wanaomzunguka na fursa alizonazo. Sisi Airtel kupitia mtandao wetu uliosambaa kote tumejipanga kukuwezesha kufikia malengo yako kupitia watu na fursa zilizokuzunguka.

"Kampeni hii inalenga kusherehekea kujitoa, ubunifu na uvumbuzi wa vijana wa Afrika na Tanzania ambayo asilimi 60 ya watu wake wana umri chini ya miaka 25.

"Kwa wateja wetu hapa Tanzania na masoko mengine, fikra chanya ni muhimu sana na kwa kufanya mambo yaende vizuri, ishi kulingana na nyakati. Tunawasaidia vijana wetu kufikiria upya nafasi zao kwa kutumia mtandao wetu kuungana na familia, marafiki, biashara na kubadilisha kila hali kuwa fursa. Tupo kwa ajili ya kufanya mawazo yatimie, tupo hapa kufungua fursa," alisema Balsingh.

Mkurugenzi wa Biashara wa Airtel Afrika, Anthony Shiner, alisema 'vijana ni muhimu katika kuiendeleza Afrika. Zaidi ya asilimia 60 ya watu barani Afrika wako chini ya miaka 25 na kwa kuwezesha kizazi hiki ni kufanya mapinduzi makubwa kwa mustakabali wa baadaye wa Afrika.

Alisema kampeni hiyo mpya kubwa zaidi kwa Airtel Afrika. Inajumuisha mfululizo wa matangazo ya runinga na mchanganyiko wa machapisho maalum kwenye kila sehemu wanayofanya biashara kwa lengo la kuendeleza ubunifu mtandaoni, na kwenye mabango kwa njia ya simu za mkononi.

# TAMISEMI yabaini mashine 2,838 PoS hazikufanya kazi miaka mitatu

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema mashine 2,838 za kukusanyia mapato (PoS) zilibainika kutokuwa hewani kwa mwaka 2018 hadi 2021 kwa halmashauri mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, TAMISEMI imefanya maboresho na matumizi ya mashine za kukusanyia mapato kupitia mfumo wa LGRCIS yatakoma ifikapo Juni 30, 2023.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Deogratius Ndejembi, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Meatu (CCM), Leah Komanya.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mashine ngapi za kukusanya mapato zilibainika kutokuwa hewani na hazikutambulika na halmashauri mwaka 2018/19, 2019/20 na 2020/21.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema kuanzia Julai mosi, 2023 hakutakuwa na PoS zitakazokuwa offline zaidi ya saa 24.

Alisema katika mwaka wa fedha 2018/19 kulikuwa na mashine 14 za PoS katika halmashauri mbili, mwaka 2019/20 kulikuwa na mashine 1,469 kwa halmashauri 54 na mwaka 2020/21 na mashine 1,355 kwa halmashauri 46 ambazo hazikuwa hewani.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), kwenye mashine hizo ilikuwa ni matumizi ya fedha mbichi na kusababisha kushuka kwa mapato ya halmashauri.

"Nilitaka kufahamu je, mfumo mpya wa TAUS unakwenda kukabiliana nayo vipi hii changamoto? Pia nataka kujua mkakati wa serikali wa kuajiri wahasibu wa kutosha katika halmashauri zetu," alihoji.

Ndejembi akijibu maswali hayo, alisema tatizo la mashine hizo kutokuwa hewani ilikuwa ni uadilifu wa watumishi na tayari serikali iliwachukulia hatua wale wote waliopatikana na hatia ya kucheza na PoS na kupoteza mapato halmashauri.

"Kwenye mfumo wa TAUS katika halmashauri zote mkurugenzi ana uwezo wa kuona makusanyo na kama kuna mashine itakuwa 'offline' Mkurugenzi atajua na TAMISEMI wanaweza kuona na Julai mosi ndio mfumo pekee utakaotumika,"alisema.

Alisema serikali imepokea ushauri wa Mbunge kuhusu kuajiri wataalamu wa taaluma hiyo.

# Upanuzi wa wingu.afrika Mashariki walipa, wasaini makubaliano kadhaa


wingu.africa group limited ("Wingu"), kampuni bobezi inayoendesha vituo vya data visivyofungamana na watoa huduma za mtandao Afrika Mashariki, inaendesha vituo vya data katika nchi nne za Djibouti, Ethiopia, Somaliland na Tanzania, na kampuni hiyo imetanua wigo wa huduma za ziada katika masoko hayo, ikiwamo uanzishwaji wa kituo cha pili kikubwa cha data nchini Djibouti. Kituo hicho kilichounganishwa na mifumo mbalimbali pamoja na kituo cha kupitishia mikongo ya mawasiliano ya chini ya bahari, kitakuwa na hadhi ya daraja la tatu (Tier -3), kisichofungamanishwa na watoa huduma wengine (carrier-neutral), na kuunganishwa na miundombinu yote ya makampuni ya mawasiliano yaliyopo nchini Djibouti sambamba na mtandao wa vituo vya data vinavyojitegemea vya Wingu unaokua kwa kasi zaidi.

Kituo hicho kitakuwa cha kwanza kwa Djibouti ambacho kinapokea takriban mikongo 11 ya mawasiliano ya chini ya bahari na ni kituo muhimu kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano kusafirishwa kwa haraka na uunganishwaji wa kimtandao.

Kutokana na mpango wake wa kuendelea kutanua wigo wa huduma zake za data, Wingu imeingia makubaliano na wateja wapya wa kimkakati, ikichagizwa na ongezeko la huduma za ukodishaji wa maeneo ya uwekaji miundombinu ya data katika vituo vyake vyote. Mikataba hii inaifanya kampuni hiyo kuwa katika nafasi ya kukidhi mahitaji ya ndani na ya kimataifa. Wingu inaruhusu watoa huduma za maudhui na watoa mafunzo ya ujengaji uwezo kuleta bidhaa na huduma zao karibu zaidi na watumiaji kama vile katika nchi zinazokua kwa kasi kiuchumi zinazohudumiwa na Wingu, ikijumuisha Tanzania na Ethiopia, yenye jumla ya watu zaidi ya milioni 200.

Ikiwa ni kampuni mwasisi wa huduma za data tangu ilipoanzisha kituo chake cha kwanza nchini Djibouti, ambacho kimekuwa kikifanya kazi kwa takriban miaka 10, Wingu ilianzisha kituo cha kubadilishana mawasiliano ya Mtandao cha kwanza nchini humo ("DjIX") na kimeendelea kuwa kituo kinachofanya vizuri barani Afrika. Kwa sasa, kupitia utaratibu unaofanana na huo lakini bunifu zaidi, Ethiopia inakwenda kuwa na kituo chake cha kwanza cha kubadilishana mawasiliano ya Mtandao ("ADDIX") ambacho kitakuwa kikiendeshwa chini ya kituo mama cha data cha Wingu kilichopo jijini Addis Ababa. Ikiwa na mkakati wake wa kusaidia kusogeza karibu huduma za mtandao za gharama nafuu, zinazoaminika, na za haraka kwa watumiaji wake katika masoko. Kampuni hiyo pia imesaini makubaliano na kituo cha kubadilishana mawasiliano ya mtandao cha Tanzania (TIX), na hivyo kituo cha tatu cha mawasiliano cha TIX kitakuwa kikiendeshwa katika kituo cha Wingu kilichopo jijini Dar es Salaam.

Kwa Djibouti, ambapo kampuni hiyo ina historia ya kujivunia na ya muda mrefu, kituo chake kipya cha data na kile cha kupokea mkongo wa mawasiliano wa chini ya bahari vitakuwa tayari kwa robo ijayo ya mwaka huu, mapema zaidi kwa ajili ya ujio wa mfumo wa kisasa duniani wa mamilioni ya fedha wa usafirishaji data kwa mkongo wa bahari utakaoletwa na kampuni hiyo. Kituo hicho kipya kinachojengwa na Wingu kwa ushirikiano na mshirika wake wa ndani TO7 Networks SAS, kilichaguliwa na ushirika unaohusika







na masuala ya mikongo ya chini ya bahari, na hii ni kwa sababu ya rekodi nzuri ya kampuni hiyo kwa Afrika na pia ni kwa kuwa kituo chenyewe hakifungamani na watoa huduma wengine na kinatoa huduma zote zile upokeaji wa mikongo ya data chini ya bahari na kupitia vituo vya data ndani ya eneo moja.

Utayari wa Wingu katika kukiendesha kituo cha Djibouti umesaidia kusainiwa kwa makubaliano mengine na kampuni ya kimataifa ya technolojia kwa ajili ya kuwafungia mifumo hiyo, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kampuni hiyo kuwapa wateja wake uzoefu wa aina yake kwa kuwasogezea maudhui karibu nao.

Wingu group limited pia inafuraha kutangaza kwamba kituo chake cha data kisichofungamana na watoa huduma nyingine za data huko Berbera, Somaliland, kinaona uhitaji wa huduma kama hizo kutoka kwa wateja wa ndani na wale wa kimataifa pia. Kwa mfano, PEACE cable, ambayo imepokelewa katika kituo hicho kwa niaba ya kampuni husika, tayari ni mteja wake na inawapa wateja wake wa Ethiopia machaguo ya ziada ya kutumia nafasi zilizopo kituoni humo kuendesha huduma za data. Wingu inaona matarijio makubwa katika soko la Ethiopia, ambalo linakua kwa kasi kufuatia mageuzi ya sekta ya mawasiliano ya simu nchini na ujio wa Safaricom kama kampuni ya pili ya mtandao wa simu. Kituo cha data cha Wingu kilichopo Addis Ababa, cha kwanza cha aina yake nchini Ethiopia, kilichaguliwa na Safaricom kuendesha vifaa vya huduma za data za kampuni hiyo na Wingu inafuraha kuunga mkono maendeleo katika soko la mawasiliano la Ethiopia.

wingu.africa
Data Ecosystems

**Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali wasiliana na**
Mr. Nicholas Lodge nicholas@wingu.africa – Afisa Mikakati Mkuu
Mr. Huneid H Ali huneid@wingu.africa – Mkurugenzi wa Wingu nchini Tanzania
Mr. Freddy Mrema freddy@wingu.africa – Mkurugenzi wa makao makuu, mauzo ya biashara na masoko.

www.wingu.africa

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suluhu ipatikane Kariakoo kazi iendelee

**MGOMO** wa wafanyabiashara wa maduka ya bidhaa mbalimbali Kariakoo, jijini Dar es Salaam, uliofanyika juzi na kusababisha maduka kufungwa, umeathiri kwa kiasi kikubwa mapato zikiwamo fedha za kigeni.

Kariakoo ni kituo kikuu cha biashara nchini ambacho kinategemewa na wafanyabiashara wa nchi jirani za Tanzania na pia wafanyabiashara wa ndani ambao wananunua bidhaa zao huko na kupeleka kwenye maduka yao.

Kusimama kwa kituo hicho, kumeathiri wageni ambao wamekuja kufuata bidhaa nchini kwa ajili ya kupeleka kwenye nchi zao.

Kitendo hicho kimewasababishia hasara kubwa, kwa kuwa kama walikuwa wamepanga kukaa nchini kwa siku chache, itawalazimu kusubiri ili kutimiza mahitaji yao hali itakayowafanya waingie gharama kuanzia ya malazi hadi chakula.

Taarifa za kuwapo kwa mgomo huo zilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii zikiwataka wafanyabiashara wote wa eneo hilo kutofungua maduka yao mpaka hapo madai yao yatakaposikilizwa na kufanyiwa kazi.

Wafanyabiashara hao walikuwa wakipinga hatua ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwataka usajili mpya wa stoo ambao unamtaka mfanyabiashara kupeleka ripoti ya mzigo uliobaki na uliouzwa.

Walidai wanapoteza wateja wengi kutoka nje wanaofuata bidhaa nchini kutokana na mambo mbali mbali ambayo yakifanyiwa kazi, taifa litapiga hatua.

Hata hivyo, TRA katika ufafanuzi kuhusu madai hayo, ilisema wamegundua mchezo mchafu unaofanyika kwamba mzigo unaweza kutolewa kwenye godauni kupelekwa kwa mteja kwa risiti moja na ikatumika siku nzima.

Serikali ilibidi iingilie kati baada ya Waziri Mkuu kutoka Dodoma na kwenda kuwasikiliza madai yao ambaye aliwasihi kufungua maduka yao kwa kuwa maduka ya Kariakoo yanategemewa na nchi nyingi na kwa kufanya hivyo kunaweza kuwafukuza wateja kutoka nje.

Kwanza tunasema hatua ya serikali kuchukua hatua mara moja ya kwenda kuwasikiliza madai yao ni kuonesha kwamba inajali wananchi wake na ipo tayari kutatua kero zao.

Jambo la msingi ni wafanyabiashara kutumia heshima hiyo waliyopewa kutii kwa kuendelea na biashara zao na kusubiri tarehe waliyopangiwa kukutana ili kufikia mwafaka.

Suala hili lisichukuliwe kirahisi rahisi kwa watu wachache kutumika ili kudumaza juhudi za serikali za kuimarisha uchumi wa nchi.

Kariakoo ni kitovu kikubwa cha biashara, hivyo sifa yake na umaarufu wake usiharibiwe na watu wachache wanaotaka kuvuruga sifa hiyo.

Pamoja na kwamba hatua ya kufunga maduka ni kushinikiza serikali kutatua kero, lakini lazima wafanyabiashara wafikirie upande wa pili wa shilingi.


Kumbukeni kuwa kufanya hivyo kunawapa fursa nchi zingine za kuwavuta wateja waliokuwa wanakuja nchini kuhamia kwenye nchi zao.

Pia, athari zinazowapata wafanyabiashara wadogo ambao walikuwa wanategemea maduka hayo kununua bidhaa na kwenda kufanyabiashara kwa ajili ya kupata kipato kinachowezesha kula na familia zao na hata kusomesha watoto wao.

Wengine kupitia biashara hizo wameweza kujenga nyumba nzuri na kuishi maisha bora. Kupitia Kariakoo, kumewafanya vijana kuacha kukaa vijiweni na kuwa wachuuzi wa vitu mitaani ambavyo vinawarahisishia wengine wasioweza kwenda Kariakoo kuvitafuta.

Hivyo, wafanyabiashara tumieni busara ya heshima mliyopewa kwa kufungua maduka na kuendelea na biashara wakati tatizo lenu likifanyiwa kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Hoja zinazoigusa jamii zisipuuzwe

**ZIPO** hoja ambazo huanzia bungeni miongoni mwa wabunge wakichangia mawazo na mijadala kuanzia bajeti za wizara mbalimbali, mabadiliko ya sheria na ripoti za kila aina ambazo ukizitafakari ndio maisha halisi ya Watanzania mijini na vijijini.

Uhalisia ni huo kwa sababu ni wawakilishi wa kijamii, wakifahamu kilichopo kwenye maeneo wanayoishi wapigakura wao wakizichunguza sekta zote kuanzia elimu, miundombinu, afya, siasa na kilimo.

Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, ni mmoja wao. Anapoanza kuchangia hoja bungeni, wabunge wenzie huanza kutabasamu, kisha kucheka kwa nguvu, utalibaini hili ukimfuatilia katika matangazo ya bungeni mubashara.

Nimemfuatilia kwa muda mrefu, hoja zake ni kama masihara lakini zimeshiba mfano mwaka 2019 alipata umaarufu mtandaoni kwa hoja kwamba elimu ya mtoto miaka mingi ni kama utumwa.

Wiki iliyopita, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewasilisha rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala Toleo la 2023, ikiwataka wadau wa sekta hiyo kutoa maoni, kuhusu yaliyomo kwenye rasimu hiyo, mojawapo ikiwa ni umri wa kuanza darasa la kwanza kuwa miaka sita, badala ya saba.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, anasema rasimu hiyo, inapendekeza umri wa kuanza ni miaka sita, kama ilivyo katika nchi nyingi duniani, huku muundo uliorekebishwa ukiruhusu mwanafunzi kukamilisha mzunguko wa masomo kwa muda wa miaka sita kwa elimu ya msingi.

Rasimu inapendekeza muundo katika mfumo rasmi wa elimu na mafunzo utakuwa mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka sita ya elimu ya msingi, miaka minne ya elimu ya sekondari ngazi ya chini, miaka miwili ya elimu ya sekondari ngazi ya juu au miaka mitatu ya amali sanifu na miaka isiyopungua mitatu ya elimu ya juu kwa kanuni ya 1+6+4+2/3+3.

Katika hili la rasimu, mapema sana Kishimba aliliona na hapa ni nukuu yake katika moja ya maelezo yake akiwa bungeni.

"Mheshimiwa mwenyekiti ukienda kwenye familia zilizoathirika na suala la elimu ukiwaambia elimu ni ufungua wa maisha, watakwambia hapana. Elimu ya Tanzania mheshimiwa mwenyekiti imekuwa kifungo cha maisha.

"Maana ni gereza gumu sana, umefungwa wewe, amefungwa mtoto na pesa zimeenda, umezeeka. Wote mna vyeti vipo ukutani...lakini muda wa kusoma vilevile watunga sera wauangalie. "Hivi nani alifanya utafiti, kwamba ubongo wa binadamu unahitaji kila mwaka darasa moja, kama yupo atuambie."

"...unachukuliwa mtoto wako kwa miaka 17 unarudishiwa akiwa na miaka 25. Mnaambiwa katafuteni kazi ya kujitegemea. Mwaka mmoja watoto wasome madarasa matatu...itatusaidia kumaliza shule mapema," anasema Kishimba.

Hoja hiyo ina mashiko kwa sababu dunia imebadilika sasa na tangu uhuru upatikane Tanzania imevuka nusu karne na mwongo mmoja. Kwa maana kwamba mabadiliko yanakwenda kwa kasi, uelewa wa binadamu unaanza mapema, kuliko enzi hizo ilikuwa mtoto kuanza shule kipimo ni kulifikia sikio upande wa pili.

Watoto wa kizazi kwenye nchi zinazoendelea nao wanakua haraka kiumbo, hususan wasichana ambao wanakumbwa na changamoto lukuki hasa mimba za ututoni.

Kwa mujibu wa wataalamu kiafya mtoto wa kike anawahi kupevuka, hata kuanzia miaka tisa, hivyo kukaa na mtoto shuleni miaka mingi ni kumuweka katika hatari ya hayo.

Mitaala inaweza ikarahisishwa na ikaeleweka kwa kipindi kifupi cha hata miezi saba hadi tisa na kikabakia kipindi kufanya marejeo yaliyofundishwa ili kuimarisha uelewa wa mwanafunzi.

Ni wakati wa Wizara ya Elimu kuchukua maoni yanayojenga jamii na si kukaa upande ambao unataka mtoto asome miaka mingi, kumbe kuna maslahi binafsi ya kibiashara ndani yake.

KESI YA KINA MDEE

## Mjumbe Bodi CHADEMA kuhojiwa mahakamani leo

**Na Grace Gurisha**

JOPO la mawakili wanaowatetea wabunge 19 wa Viti Maalum wanaodaiwa kuingizwa bungeni kinyume cha sheria katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wao, leo linatarajiwa kumhoji Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Lucy Mollel.

Mawakili wanaounda jopo hilo ni Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu, Emmanuel Ukashu, Joyce Mwakakila na Afrey Maunga. Watamhoji mjumbe huyo mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam.

Mollel ataulizwa maswali kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani katika kesi iliyofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18, wakiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Machi 10, 2023, Prof. Azaveri Lwaitama ambaye ni mjumbe wa bodi hiyo wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa jopo hilo, alidai kuwa Mdee na wenzake 18 wakitoka bungeni, atakuwa wa kwanza kuwatetea kurudishwa katika chama kama wakifuata utaratibu.

Mjumbe huyo alidai Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alishaweka wazi kwamba alimwita Mdee Nairobi, Kenya ili kuzungumza naye kwa kile ambacho wamekifanya kwa sababu yeye (Mdee) ndiye alikuwa kiongozi wa wenzake kutokana na ushawishi mkubwa aliyokuwa nao.



Alidai kuwa katika mazungumzo hayo na Mbowe, Mdee alilia, hivyo wakitoka bungeni, atakuwa mtu wa kwanza kuwatetea kurudishwa kwenye chama kwa sababu shida sio ubunge wao bali utaratibu hakufuatwa.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022, wakiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba kuwekwa zuio Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naTume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote dhidi yao hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.



Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Willa Haonga (wa tatu kushoto), akikabidhi vifaa tiba kwa Dk. Eliya Nixon Mwakibete wa Kituo cha Afya Kidodi (wa pili kulia), ikiwa ni sehemu ya msaada uliotolewa na kampuni hiyo, kwa vituo vya afya Mkamba, Nyandeo na Kidodi, wilayani Kilombero na Kilosa, mkoani Morogoro kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Tuhuma ufisadi mamilioni ujenzi soko la machinga zazua balaa

**Na Moses Ng'wat,**
TUNDUMA

HALMASHAURI ya Mji wa Tunduma imewasimamisha kazi Ofisa Ununuzi wa Halmashauri hiyo, Ibrahim Lulimo na Mhandisi wa Ujenzi, Japheti Chota, kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa soko la wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, ambalo serikali ilishatoa Sh. milioni 383.

Ujenzi wa soko hilo ambalo linajengwa katika Kata ya Majengo mjini Tunduma umesimama kwa muda mrefu. Sababu kuu inayotajwa hakuna fedha katika akaunti ya utekelezaji wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Philemon Magesa, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, kuwa alichukua hatua ya kuwasimamisha kazi maofisa hao baada ya ripoti ya Mkaguzi wa Ndani kubaini kuwapo taarifa za vifaa vilivyonunuliwa lakini havikupelekwa eneo la mradi. "Mkaguzi wa Ndani alishafanya ukaguzi katika mradi huu. Baadhi ya dosari zilizoonekana kwenye mradi huu ni baadhi ya vifaa kununuliwa lakini havikuonekana eneo la mradi ambavyo ni nondo, saruji, mchanga, kokoto na mawe.

"Na hatua nilizochukua ni kuwasimamisha baadhi ya watumishi ambao ni Ofisa Ununuzi na Mhandisi aliyekuwa anasimamia," alisema Magesa.

Alifafanua kuwa baada ya kuwasimamisha kazi maofisa hao, alikabidhi suala hilo kwa Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fakh Lulandala, ili achukue hatua zaidi kwa kuwa yeye ana vyombo vya dola.

Baada ya maelekezo hayo ya mkurugenzi, Mkuu wa Mkoa alimtaka mkuu wa wilaya atoe ufafanuzi wa hatua alizochukua baada ya kukabidhiwa majina ya maofisa hao waliosimamishwa.

Mkuu wa Wilaya Momba, Lulandala, alisema kuwa baada ya kukabidhiwa majina hayo, aliwakamata wahusika na kuwakabidhi kwa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kituo maalum cha Tunduma ili achunguze zaidi suala hilo.

Ofisa wa TAKUKURU kituoni huko, Benedict Kaombwe aliyeitwa na Mkuu wa Mkoa ili kutoa ufafanuzi wa hatua zilizochukuliwa na taasisi hiyo, alijibu kwa kifupi kuwa uchunguzi unaendelea.

Majibu hayo ya Ofisa wa TAKUKURU hayakumfurahisha Mkuu wa Mkoa ambaye alihoji "inakuwaje suala hilo ambalo tayari ripoti ya Mkaguzi wa Ndani imeeleza bayana uchunguzi wake uchukue zaidi ya miezi miwili?

"TAKUKURU uchunguzi zaidi ya miezi miwili ujue hizi ni fedha za umma. Mnachunguza nini halafu mbaya zaidi hadi Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya inachukua hatua... hapana! Hapa lazima pana vitu haviko sawa.

"Ninakuelekeza vinginevyo nitaongea na wakubwa zako huko. Umepewa kazi ya kuwachunguza watu kwa tuhuma za ubadhirifu. Ninataka haraka tupate majibu kwani hizi ni fedha zilizotolewa na Rais kwa ajili ya machinga, sasa nyie hapa Tunduma mnaona mmeletewa hela za kula?

"Haiwezekani uchunguze zaidi ya miezi miwili wakati mkaguzi ameshatoa ripoti yake," Dk. Michael alisisitiza na kuiagiza TAKUKURU kupeleka haraka ripoti yao ya uchunguzi ofisini kwake pamoja na ripoti ya Mkaguzi wa Ndani.

Dk. Michael pia alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya kuwatafuta watuhumiwa wa ubadhirifu huo na kuwahoji ili hatua za kisheria zianze kuchukuliwa dhidi yao.

Pia aliwataka Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kuhakikisha watu wote wanaofanya ubadhirifu katika wilaya hiyo wasifumbiwe macho na badala yake washughulikiwe kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Mradi wa Soko la Machinga katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma unajengwa katika Kata ya Majengo mjini Tunduma, ukitarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni sita. Tayari serikali imeshatoa Sh. milioni 383 na halmashauri kupitia mapato ya ndani imeongeza Sh. milioni 28 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima na mfumo wa umeme. Sasa ujenzi umesimama na hakuna salio lolote katika akaunti ya mradi huo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Ummy ajivunia uwekezaji mkubwa wa sekta afya

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya ili Watanzania wapate huduma zilizo bora na kulipia kabla ya kuugua.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akihitimisha hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24.

"Bima ya Afya kwa wote ndiyo itakayotutoa, tumefanya uwekezaji mkubwa katika huduma za afya, tumejenga ili wananchi wapate huduma bora, inabidi waweze kulipia kabla ya kuugua, suala hili tunaendelea na majadiliano ndani ya kamati na tunaamini tutaweza kufikia muafaka," alisema wakati akizungumzia suala la Bima ya Afya.

Alisisitiza kwamba Bima ya Afya ndiyo roho ya huduma ya afya na kufafanua kuwa asilimia 70 ya fedha za hospitali za umma na binafsi zinategemea Bima ya Afya.

"Tumefanya utafiti na kuona baadhi ya vifurushi vinahatarisha uhai na uendelevu wa Mfuko wa Bima ya Afya. Hawa watoto wa afya kadi wanachangia Sh. 50,400 katika kila Sh.100 wanatumia Sh. 667, la pili tumefanya uchambuzi zaidi, mwaka 2020/21 watoto waliosajiliwa Toto Card walikuwa ni 157,920 walichangia Sh. bilioni 5.9 wakatumia Sh. bilioni 40.5, jamani kuna Bima ya Afya hapo," alihoji.

Waziri Ummy alisema fedha zinapokwenda ni kwamba asilimia 53 ni kumwona daktari.

"Watanzania tuna utamaduni fulani, nikishakuwa na bima ya afya ninakwenda kwenye kliniki ya kumuona daktari bingwa, tukaangalia magonjwa gani haya. Ugonjwa wa kwanza ni malaria ambao unatibiwa katika zanahati, ugonjwa wa pili mfumo wa hewa unatibiwa zahanati.

"Ugonjwa wa tatu UTI inatibiwa katika ngazi ya chini, tumeangalia asilimia 58 za fedha za Toto Card zimekwenda kwenye vituo binafsi na asilimia 20 imekwenda hospitali za serikali na asimilia 22 imekwenda katika vituo vya taasisi za dini," alisema.

Alisema hakuna uendelevu wa bima ya watoto Afya Card ndiyo maana wanasema kuna vifurushi, ili kundi hilo lisajiliwe pamoja na wazazi wao ama shuleni ili kama shule ina watoto 100 watakoumwa labda watakuwa 10 na waliobaki watawalipia wenzao.

"Tuilinde sana NHIF Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI) fedha inazokusanya taslimu ni Shilingi bilioni tano na NHIF analipwa Sh. bilioni 22 kwa mwaka, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) fedha anazozikusanya taslimu ni Sh. bilioni 12 na NHIF Sh. bilioni 50, fedha hizi ndizo mnatupa maombi kuna mgonjwa amekwama Muhimbili, JKCI nadaiwa maiti ndiyo zinatumika kulipia wagonjwa wetu," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebecca Msemwa (kulia), akishirikiana na Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdala Shaib Kaim kumtwisha ndoo ya maji mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kauzeni, baada ya kuzindua mradi wa maji unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA). kwenye kata ya Kauzeni, wilayani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Mahakama yakataa maombi ya DPP utekelezaji hukumu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetupilia mbali maombi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya kutaka kupinga mwenendo wa utekelezaji wa hukumu iliyotolewa, ikimtaka Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Isack Kihwili, kuilipa Kampuni ya Coast Textiles Ltd Sh. bilioni 145.9.

Jaji Amir Mruma amemwagiza Kihwili kutii amri iliyotolewa, inayomtaka yeye binafsi na sio mwakilishi wake kufika mahakamani kujieleza kwanini hajatekeleza hukumu ya mahakama iliyotolewa zaidi ya miaka saba iliyopita.

Jaji Mruma alisema anakataa ombi la Wakili Mkuu wa Serikali la kusitisha mwenendo wa kukazia hukumu hiyo na kusisitiza Kihwili anapaswa kufika mwenyewe ili kuonyesha sababu kwanini hajatekeleza amri hiyo.

"Fedha hizo zinazoonyeshwa wenye hukumu sio za serikali, bali ni za Benki ya FBME, hivyo Sheria ya Mashauri ya Serikali, kama ilivyowasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Jacline Kinyasi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, haiwezi kutumika," alisema Jaji Mruma.

Jaji Mruma alisema Wakili Mkuu hatakiwi kuchanganya kati ya amri inayotolewa dhidi ya serikali na amri ambayo ni dhidi ya mtu binafsi, ambaye mali yake iko chini ya ulinzi wa ofisa wa umma, kama Kihwili, ambaye anashikilia fedha hizo kwa sababu ya kuwa mfilisi wa FBME Bank Ltd.

Pia Jaji Mruma alikataa ombi la wakili huyo la kutaka kusimamisha mwenendo huo wa kukazia hukumu kwa sababu mahakama tayari imeshaamua shauri hilo. Wakati wa kusikiliza maombi hayo, Kinyasi alidai kuwa ingawa hawapingani na hukumu iliyotolewa, kampuni hiyo ilipaswa kufuata utaratibu uliowekwa chini ya Sheria ya Mashauri ya Serikali ili kutekeleza mchakato wa kukazia hukumu ya mahakama.

Alidai kuwa chini ya Sheria ya Mashauri ya Serikali, Coast Textiles Ltd ilitakiwa kuwasilisha cheti katika Wizara ya Fedha kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili kutekeleza malipo hayo kwa kuwa Kihwili ni mtumishi wa umma. Pia aliiomba mahakama kusitisha utekelezaji wa hukumu hiyo kwa sababu wamewasilisha taarifa ya rufani na kuomba kibali cha kukata rufani dhidi ya amri iliyotolewa na Jaji Mruma Mei 20, 2022 ya kumtaka Mkurugenzi wa DIB kulipa kiasi hicho cha fedha.

Wakili Joseph Rutabingwa wa Kampuni ya Costile alidai kuwa uamuzi uliotolewa na Jaji Mruma Mei 21, 2022 ulikuwa wa mwisho na hadi wakati huo Kihwili alikuwa tayari amewasilisha hati ya kiapo kueleza kwanini hakutekeleza hukumu ya mahakama na uamuzi kuhusu hoja hiyo iliyotolewa.

"Katika mazingira haya yeye (Kahwili) hawezi kupewa nafasi nyingine ya kueleza jambo lilelile. Kilicho mbele ya mahakama kwa sasa ni kueleza kwanini asifungwe gerezani kwa kushindwa kutekeleza hukumu ya mahakama?" Alidai wakili huyo.

Mei 21, 2022, Jaji Mruma alitoa amri hiyo dhidi ya Mkurugenzi wa DIB, mlalamikiwa, ambaye aliteuliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuwa Mfilisi wa Benki ya FBME baada ya kuridhia maombi ya utekelezaji wa hukumu yaliyowasilishwa na Costal Textiles Limited, mwombaji.

Jaji alibainisha zaidi kuwa hakuna sababu zilizotolewa na mfilisi kuonyesha ni kwanini benki husika ilifungwa na baada ya hapo kunyang'anywa leseni yake ya uendeshaji.

## Umiliki ardhi changamoto wanawake wazawa Afrika

**Na Jenifer Gilla,** BRAZZAVILLE

KUTOKUMILIKI ardhi kisheria kumeelezwa kuwa moja ya changamoto zinazorudisha nyuma juhudi za wanawake wazawa katika kuhifadhi rasilimali zilizoko katika maeneo wanayoishi.

Changamoto nyingine zimetajwa kuwa ni kutofikiwa na fedha za maendeleo zinazotolewa na wadau, kutokuwapo mikakati madhubuti ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, kusajiliwa na kutambulika kama watoa tiba za asili.

Mkurugenzi wa Programu wa shirika lisilo la kiserikali la Right Resources Initiative (RRI) Afrika, Patrick Kipalu, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifunga kongamano la uhamasishaji wa ushiriki wa wanawake wazawa Afrika Mashariki na Bonde la Congo katika uhifadhi wa bioanuai lililofanyika Brazzaville, Jamhuri ya Congo, lililoandaliwa na Shirika hilo kwa kushirikiana na la REPALEAC.

Alisema umiliki wa ardhi kisheria ni moja ya mahitaji muhimu ya wazawa ni nguzo ya kuimarisha maisha ya jamii, kuwapa uhuru wa kuamua kuhusu rasilimali zao, ikiwamo namna wanavyotaka kuzitumia ili kujikwamua kichumi na kufikia malengo ya maendeleo waliyojiwekea, pia inachangia kulinda utamaduni na mtindo wa maisha wa jamii yoyote.

"Utafiti unathibitisha kwamba usalama wa ardhi unapohakikishwa kwa jamii, uhifadhi wa rasilimali katika jamii unakuwa mkubwa na ukataji wa miti unafanyika kwa viwango vya chini," alisema Patrick.

Mratibu wa Kanda ya Afrika ya Kati la REPALEAC, Joseph Itongwa, alisema licha ya umiliki wa ardhi kuwa ni msingi wa kitamaduni na utulivu wa wanawake katika maeneo yao, bado ni changamoto kubwa inayohitaji serikali kuingilia kati ili kuitatua.

Alisema suala hilo linarudisha nyuma jihitahada za wadau wa maendeleo, ikiwamo mashirika yanayotetea haki za wazawa za kusaidia jamii hizo kuhifadhi maliasili zao kutokana na hofu iliyotanda ya kuondolewa katika maeneo yao.

Aidha, amewaomba wadau hao kuendelea kuwaunga mkono katika juhudi zao za kupigania haki za kumiliki ardhi kisheria pamoja kuwapa fedha za mitaji ya biashara ili waendelee kunufaika na rasilimali zinazowazunguka.

Kiongozi wa jamii ya Bantwa kutoka nchini Rwanda, Marthe Muhawenimana, alisema kutokuwa na umiliki wa ardhi kisheria kunawafanya waishi kwa wasiwasi kuwa siku yoyote wanaweza kuodolewa katika maeneo hayo hali inayodhorotesha ushiriki wao katika kuhifadhi maliasili.

Alisema hofu hiyo imeongezeka miaka ya hivi karibuni baada ya kutokea visa vya wazawa kuondolewa na serikali katika maeneo yao na kupelekwa katika maeneo mageni kwa kisingizio cha kupisha shughuli za uhifadhi jambo analoona sio sababu yenye nguvu.

"Tumeshuhudia wenzetu nchi jirani ikiwamo Ngorongoro nchini Tanzania, wakiondolewa katika makazi ya yao ya asili na kupelekwa ugenini ili kupisha shughuli za uhifadhi wa utalii, jambo linalotukosesha amani kuwa na sisi muda wowote tunaweza kuondolewa kwa kuwa hatuna umiliki halali," alisema Marthe.

Mtaalam wa elimu ya wazawa, Marie Dorothee Bafalikike kutoka Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema changamoto nyingine wanayokumbana nayo ni ubaguzi na kutofikiwa kwa fedha zinazotolewa na wadau wa maendeleo kwa ajili ya jamii zao.

Aliwataka wadau wa maendeleo wanaotoa fedha za kusaidia maendeleo ya jamii za wazawa kuwa na mpango mkakati utakaosaidia kufahamu kama pesa wanazotoa zinawafikia wahusika waliowalenga, kwa sababu mara nyingi zimekuwa zikiwanufaisha watu wasio watarajia.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24



**Mhe. Prof. Adolf F. Mkenda (Mb)**
WAZIRI



**Mhe. Omari Juma Kipanga (Mb)**
NAIBU WAZIRI WA ELIMU



**Dkt. Franklin Jasson Rwezimula**
NAIBU KATIBU MKUU



**Prof. Carolyne Ignatius Nombo**
KATIBU MKUU



**Prof. James Epiphany Mdoe**
NAIBU KATIBU MKUU

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24

**A. UTANGULIZI**

**1.** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**2.** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2023/24.

**3.** Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na kutimiza miaka miwili tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho ametuongoza vyema na kutuwezesha kupata maendeleo na mafanikio makubwa kutokana na miongozo anayotupatia ambayo imetusaidia sana katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, namshukuru kwa kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kuongoza Wizara hii.

**4.** Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri katika kuliongoza Taifa letu.

**5.** Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa uongozi wenu mahiri wa kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa jimbo la Babati Vijijini, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa jimbo la Mufindi Kusini, kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**6.** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb), Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati. Aidha, naomba niwashukuru kwa kupokea, kuchambua na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/23 na kuishauri vema Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2023/24. Natambua na kuthamini sana mchango wa Kamati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Elimu inachangia katika utekelezaji wa Mpango wa III wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26 kwa kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi, maarifa na stadi zitakowezesha kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

**7.** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu Beatrice kwa kuendelea kuwa karibu yangu na kunitia moyo na kuniwezesha kufanya kazi kwa juhudi na ari kubwa.

**8.** Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

**B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

**9.** Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi **1,555,827,466,796.00** kwa ajili ya FUNGU namba 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo Shilingi **533,456,916,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **1,022,370,550,796.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi **2,709,163,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha Shilingi **1,176,870,000.00** za mishahara na Shilingi **1,532,293,000.00** za matumizi mengineyo.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

**10.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya Shilingi **642,667,620,483.06** ambapo kiasi cha Shilingi **8,680,995,000.00** kilipangwa kukusanywa na idara na vitengo na Shilingi **633,986,625,483.06** zilipangwa kukusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni kutokana na ada, malipo ya ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

**11.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2023 Wizara imekusanya **Shilingi 400,139,396,734.49** sawa na asilimia **62** ya makadirio ambapo **Shilingi 8,116,780,685.14** zimekusanywa na idara na vitengo na **Shilingi 392,022,616,049.35** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Matumizi ya Kawaida**

**12.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 533,456,916,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya mishahara ni **Shilingi 500,196,732,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 80,090,663,000.00** na Taasisi ni **Shilingi 420,106,069,000.00**) na Matumizi Mengineyo **Shilingi 33,260,184,000.00** (idara na vitengo **Shilingi 25,558,821,658.00** na Taasisi **Shilingi 7,701,362,342.00**).

**13.** Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 410,266,920,334.60** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na **asilimia 76.91** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,979,133,163.28** sawa na **asilimia 73** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Miradi ya Maendeleo**

**14.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,022,370,550,796.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 840,906,789,796.00** na fedha za nje ni **Shilingi 181,463,761,000.00.**

**15.** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,063,782,313,215.36** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **104.05** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 880,846,253,860.91** ni fedha za ndani na **Shilingi 182,936,059,354.45** ni fedha za nje.

**16.** Mheshimiwa Spika, ongezeko la kiasi cha fedha za ndani kilichopokelewa kinajumuisha: kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vishikwambi vya walimu, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, na wathibiti ubora wa shule; na Fedha kwa ajili ya Bodi ya Mkopo kilichoongezewa ili kukidhi mahitaji ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha, ongezeko la kiasi cha fedha za nje kilichopokelewa kinajumuisha fedha zilizopatikana kutokana na matokeo ya kutekeleza kwa ufanisi kwa viashiria vya miradi ya lipa kulingana na matokeo (Program for Results).

**C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**17.** Mheshimiwa Spika, pamoja na mapitio ya sera na mapitio ya mitaala, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23, ulijielekeza katika kutekeleza maeneo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na: (i) kuongeza fursa na kuimarisha elimu ya ufundi nchini; (ii) kuhimiza uandishi, uchapishaji na uchapaji wa vitabu hapa nchini; (iii) kuongeza wigo wa shule za ufundi; na (iv) kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo katika taasisi za Elimu ya Juu kwa kuanza kujenga kampasi za vyuo zenye kujielekeza katika mafunzo kwa vitendo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**18.** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo hayo ya kimkakati ulieenda sambamba na utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

**a. Kuhuisha Sera, Mitaala, Sheria na Miongozo ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo Nchini**

**19.** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Mitaala katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Juu kwa lengo la kuleta mageuzi ya elimu nchini na kuwapatia wahitimu ujuzi na maarifa stahiki.

**20.** Mheshimiwa Spika, uhuishaji wa Sera unahusisha mabadiliko katika mfumo wa elimu ili kuwawezesha wahitimu kujiamini, kujiajiri na kuajirika katika mazingira ya utandawazi na kukidhi mahitaji ya soko. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ili kubaini utoshelevu wa sera hiyo na kuandaa taarifa ya mapitio ambayo imewezesha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 - Toleo la mwaka 2023 ambalo limejielekeza katika utoaji wa elimu ya amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Vilevile, imefanya mapitio ya mitaala ili kubaini utoshelevu wake na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya mitaala kulingana na maelekezo ya sera.

**21.** Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu inapata maoni ya wadau wengi kabla ya uidhinishwaji wake, Wizara imeendesha Kongamano la Kitaifa lililofanyika kuanzia **tarehe 12 hadi 14 Mwezi Mei, 2023** Mkoa wa Dodoma. Katika Kongamano hilo, zaidi wa Wadau wa Elimu 1,450 walishiriki (walioshiriki moja kwa moja ukumbini 1,200 na walioshiriki kwa njia ya mtandao 250) wakiwemo wanafunzi, walimu, wahadhiri, wakufunzi, wazazi, wadau wa maendeleo na viongozi mbalimbali ikiwa ni pamoja na viongozi wa dini, siasa na kijamii. Vilevile, Wizara inaendelea kupokea maoni hadi tarehe 31 Mei, 2023. Aidha, mwezi Juni, 2023 Wizara itaanza utaratibu za kuomba idhini ili kuwezesha utekelezaji wake.

**22.** Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Elimu ya Awali, Msingi na Elimu ya Ualimu inatolewa kwa kuzingatia viwango na ubora stahiki, Serikali imeandaa miongozo kama ifuatavyo:

(i) Mwongozo wa Kitaifa wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya awali kwa kuzingatia viwango vya ubora pamoja na kiongozi cha kutekeleza mwongozo husika;

(ii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo Shikizi vya Shule ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika vituo shikizi nchini; na

(iii) Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Utekelezaji wa Shughuli za Ushirikiano wa Wazazi na Walimu katika Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya wazazi na walimu katika kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi.

**b. Kuongeza Fursa za Elimu kwa Wote**

**23.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum. Aidha, inaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi waliopata fursa za masomo wanashiriki kikamilifu katika masomo na kuhitimu. Azma hiyo, imefikiwa kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo:

(i) usajili wa jumla ya asasi 683 zilizokidhi vigezo kati ya 684 zilizoomba kwa mchanganuo ufuatao: shule za Awali pekee 26 zisizo za Serikali, shule za Awali na Msingi 309 (Serikali 150 na zisizo za Serikali 159) na Sekondari 346 (Serikali 209 na zisizo za Serikali 137) na Vyuo vya Ualimu viwili visivyo vya Serikali ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini;

(ii) imesajili jumla ya wanafunzi 22,802 (Wanawake 11,641 na Wanaume 11,161) katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ambapo Astashahada ya Elimu ya Msingi ni 15,177 (Wanawake 8,406 na Wanaume 6,771), Stashahada ya Ualimu 2,787 (Wanawake 1,076 na Wanaume 1,711) na Stashahada maalum ya ualimu wa sayansi sekondari wa miaka mitatu 4,838 (Wanawake 2,159 na Wanaume 2,679); na

(iii) imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uandikishwaji na umuhimu wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia vyombo ya habari, mitandao ya kijamii na maadhimisho ya Siku ya walemavu duniani, Wiki la Elimu Jumuishi, Siku ya Fimbo nyeupe kwa wasioona, Siku ya Braille duniani, na Siku ya watoto wenye Downsyndrome na Rare Disease.

**24.** Mheshimiwa Spika, katika kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali imewezesha kuwarejesha wanafunzi 1,967 (Wanawake 1,046 na Wanaume 86) katika Mfumo Rasmi wa Elimu. Vilevile, imedahili jumla ya wanafunzi 23,263 (Wanawake 15,006 na Wanaume 8,257) katika mikoa 26 ambao wanapata Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala (Alternative Education Pathway).

**25.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ujenzi wa shule mpya za msingi 40; madarasa 174 katika shule za msingi 70; mabweni manne katika shule za msingi tatu; nyumba za walimu 53 katika shule za msingi 53; mabweni manne katika shule za msingi nne; matundu ya vyoo 6,634 katika shule za msingi 472 na ofisi moja. Aidha, imewezesha ukarabati wa shule kongwe 45 za msingi; na

(ii) imewezesha ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya za sekondari 231 za Kidato cha 1 hadi cha 4 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule, shule 10 za Kidato cha 5 na 6 kwa wanafunzi wa kike kati ya shule 26 zinazotarajiwa kujengwa kwa kila Mkoa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila shule. Aidha, imewezesha ujenzi wa madarasa 46 katika shule za sekondari 46; mabweni 72 katika shule za sekondari 54 nyumba za walimu 19 katika shule za sekondari 18; maabara 26 katika shule za sekondari 14, maktaba nne, mabwalo 22, ofisi sita. Vilevile, imewezesha upanuzi wa shule kongwe 18 na ukarabati wa shule kongwe 16 za sekondari.

**26.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu tarajali kwa kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Ualimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa ambapo ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji. Vilevile, imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vitano ambavyo ni; Mamire, Vikindu, Songea, Singachini na Katoke. Ujenzi na ukarabati huo upo katika hatua za ukamilishaji. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya ualimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ualimu; na

(ii) imekamilisha ukarabati wa Chuo cha Ualimu Butimba na kuendelea na ukarabati wa maabara za Sayansi na TEHAMA katika vyuo sita vya ualimu ambavyo ni; Chuo cha Ualimu Morogoro, Mpwapwa, Tukuyu, Kasulu, Patandi na Dakawa. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**27.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali imenunua na kusambaza vitimwendo 253 kwa wanafunzi wa shule za msingi 200 na sekondari 53 wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuwawezesha kumudu mazingira ya shule na nyumbani.

**c. Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu**

**28.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kufanya tathmini ya jumla katika asasi 6,317 (Awali na Msingi 5,351, Sekondari 932 na Vyuo vya Ualimu 34) ambapo shule zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa ofisi tano za Uthibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Ubungo, Njombe, Bunda na Tarime kwa lengo la kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.

**29.** Mheshimiwa Spika, katika kujenga umahiri wa walimu na wakufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa shule na vyuo vya ualimu, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa moduli 12 za Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) wa Elimu ya Awali na Msingi na imetoa mafunzo kwa walimu 26,657 wanaofundisha elimu ya awali na msingi kupitia vituo vya walimu na shule teule;

(ii) imetoa mafunzo kuhusu Elimu ya Stadi za Maisha zinazolenga afya ya uzazi, VVU na UKIMWI na Jinsia kwa walimu 25,700 kati ya walimu 27,750 wa shule za msingi na sekondari waliolengwa ili kuwajengea uwezo wa kufundisha masuala mtambuka. Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu darasa jumuishi kwa walimu 17,800 kati ya walimu 20,000 waliolengwa wanaofundisha Darasa la I – IV. Mafunzo yalilenga kuimarisha utekelezaji wa mitaala; na

(iii) imetoa mafunzo kuhusu mbinu bora ya ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa vitendo kwa walimu wa sekondari 15,282 (Wanawake 3,985 na Wanaume 11,297) kati ya walimu 20,000 waliolengwa. Aidha, mafunzo kwa walimu 4,718 waliobaki yanaendelea kutolewa.

**30.** Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha ufundishaji wa masomo ya Amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi) kwa elimu ya msingi na sekondari kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa Sera na Mtaala Mpya, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeanza maandalizi ya Elimu ya Ualimu wa Ufundi kwa kubainisha vifaa na mashine zinazohitajika katika mafunzo hayo; na

(ii) imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu wa Ufundi na kubainisha Vyuo vya Ualimu 10 ambavyo vitatekeleza mtaala huo. Vyuo hivyo ni; Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara (U), Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga.

**31.** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha upatikanaji wa vitabu kwa mwanafunzi katika elimu ya awali, msingi na sekondari ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na uchapaji wa vitabu 2,000,000 vya masomo ya Sayansi na Hisabati kwa ajili ya kusambaza katika Halmashauri zenye upungufu mkubwa;

(ii) imechapa na kusambaza nakala 12,307,578 za vitabu kwa mchanganuo ufuatao: nakala 2,535,564 za vitabu vya hadithi vya Elimu ya Awali; nakala 3,885,000 za Vitabu vya Hadithi vya Darasa la I - II; nakala 4,181,226 za vitabu vya Kiada Darasa I na II; nakala 1,687,140 za Vitabu vya Kiada vya Darasa la III, IV na V; nakala 17,104 za Vitabu vya Maandishi yaliyokuzwa Darasa la III, IV na V kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu; nakala 640 za Vitabu vya kiada vya maandishi ya breli kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali wasioona; na nakala 904 za maandishi yaliyokuzwa kwa wenye uoni hafifu; na

(iii) imechapa na kusambaza nakala 525,000 za vitabu vya kiada vya masomo ya Mathematics, Agriculture, English Baseline Orientation course, Biology, Chemistry, Book keeping, Civics, English, Food and Human Nutrition, French, Geography, History, Information and Computer Studies, Kiswahili, Economics, Music, Physics, Textiles and Theatre Arts kwa kidato cha 1 – 6.

**32.** Mheshimiwa Spika, vitabu vyote vilivyochapwa na kusambazwa vinapatikana katika Maktaba Mtandao ambapo wanafunzi na walimu wanaweza kuvipata bila gharama yoyote ya kuunganishwa kwa mtandao (Zero - Rating) na hivyo kurahisisha upatikanaji wake.

**33.** Mheshimiwa Spika, imesimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi bunifu ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Rais Mstaafu wa Msumbiji, Mhe. Joaquim A. Chissano. Tuzo hiyo imehusisha mashindano ya uandishi wa riwaya na mashairi ambapo jumla ya miswada 283 (Riwaya 85, Ushairi 193 na nje ya nyanja za kushindaniwa 5) ilipokelewa.

**34.** Mheshimiwa Spika, katika Tuzo hiyo, mshindi wa kwanza kwa kila nyanja alizawadiwa fedha taslimu **Shilingi 10,000,000.00**, ngao, cheti pamoja na vitabu vyao kuchapwa na kusambazwa kwa gharama ya Serikali. Mshindi wa pili alizawadiwa **Shilingi 7,000,000.00** na cheti na mshindi wa tatu **Shilingi 5,000,000.00** na cheti kwa kila nyanja. Vilevile, tuzo hiyo itasaidia kuongeza idadi ya vitabu vilivyoandikwa na Watanzania badala ya kutegemea vitabu vinavyotoka nje ya nchi.

**35.** Mheshimiwa Spika, katika kukuza ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini pamoja na kutambua, kuibua, kukuza vipaji vya uandishi na kuongeza ari ya usomaji nchini, Serikali imeratibu mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi 1,116 wa shule za sekondari ambapo washindi watano walipatikana kwa ajili ya kushiriki katika mashindano ngazi ya Kikanda.

**36.** Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutoa huduma ya maktaba nchini kwa ajili ya kupata maarifa na taarifa mbalimbali, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imesambaza nakala za vitabu 21,200 katika maktaba za mikoa 20.

**37.** Mheshimiwa Spika, katika eneo la upimaji na tathmini ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) kwa mwaka 2022 kwa wanafunzi **1,592,600** ambao ni sawa na asilimia **92.65** ya wanafunzi **1,718,896** waliosajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne. Katika mtihani huo wanafunzi **1,320,700** sawa na asilimia **82.95** walifaulu;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) wa mwaka 2022 kwa watahiniwa **1,350,881** ambao ni sawa na asilimia **97.59** ya watahiniwa **1,384,186** waliosajiliwa. Katika mtihani huo watahiniwa **1,073,402** sawa na asilimia **79.62** walifaulu;

(iii) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2022 kwa wanafunzi **635,130** ambao ni sawa na asilimia **92.00** ya wanafunzi **690,341** waliosajiliwa. Katika mtihani huo wanafunzi **539,645** sawa na asilimia **85.18** walifaulu;

(iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) wa mwaka 2022 kwa watahiniwa **522,217** ambao ni sawa na asilimia **97.66** ya watahiniwa **534,753** waliosajiliwa. Katika mtihani huo watahiniwa **456,975** sawa na asilimia **87.79** walifaulu;

(v) imeendesha Mtihani wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa **9,557** kati ya watahiniwa **12,110** waliosajiliwa kufanya mtihani ambapo watahiniwa **4,059** sawa na asilimia **42.47** walifaulu; na

(vi) inaendelea na utahini wa Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE), 2023 kwa watahiniwa **106,946** waliosajiliwa na Mtihani wa Ualimu kwa watahiniwa **8,900** waliosajiliwa. Mitihani hiyo ilianza kufanyika tarehe 2 Mei, 2023.

**d. Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Utoaji wa Elimu na Mafunzo katika Ngazi Zote za Elimu Nchini**

**38.** Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa mafunzo kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (Education Sector Development Plan) na Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan) 2021/22 – 2025/26 kwa wadau mbalimbali 1,221 wakiwemo Maafisa Elimu Mkoa na Wilaya; Maafisa Mipango; Wakurugenzi wa Halmashauri; Wakuu wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mkoa na Wilaya; Wathibiti Ubora wa Shule Wakuu na Wakuu wa Vyuo. Mafunzo yalilenga kujenga uelewa kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu Nchini na kujumuisha mpango huo katika mipango na bajeti za elimu kwa ngazi ya Halmashauri na Mkoa.

**39.** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuimarisha usimamizi wa elimu nchini, Wizara imesambaza jumla ya vishikwambi 4,067 kama ifuatavyo: vishikwambi 1,352 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu; 305 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; 730 kwa wakufunzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; na 1,680 kwa Wathibiti Ubora wa Shule Ngazi ya Kanda na Halmashauri. Aidha, imekabidhi vishikwambi 274,812 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na vishikwambi 6,600 kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ili visambazwe kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, maafisa elimu ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata.

**e. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Mafunzo ya Amali)**

**40.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 123,352 (Wanawake 65,894 na Wanaume 57,458) katika Ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada kwa fani mbalimbali; na

(ii) imesajili vyuo 127 katika Bodi za Masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyuo vitatu; Biashara, Utalii na Mipango vyuo vinne; Sayansi na Teknolojia Shirikishi chuo kimoja na vyuo vya ufundi stadi (VET) 119; na kufanya jumla ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuwa 1,329 (Vyuo vya Elimu ya Ufundi -TET 465, Vyuo vya Ufundi Stadi - VET 809 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC 55).

**41.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika taasisi za Elimu ya ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kuhusu upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 1,206 wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji; na

(ii) imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,980 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa wadau.

**42.** Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa na ubora wa elimu ya ufundi, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo lenye madarasa nane yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 880 kwa wakati mmoja, maabara sita zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 270 kwa wakati mmoja, bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 428 kwa wakati mmoja na ofisi 26 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 104 katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(ii) inaendelea na ujenzi wa hosteli katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 45. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa jengo la Maktaba itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika chuo hicho; na

(iii) inaendelea kukamilisha ujenzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Wilaya 25 ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Aidha, Chuo cha Wilaya ya Mbarali na Chuo cha Wilaya ya Kishapu vimeanza kutoa mafunzo.

**f. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

**43.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza fursa za Elimu na Mafunzo ya

Elimu ya Juu nchini kwa kudahili jumla ya wanafunzi wa Elimu ya Juu 113,383 (Wanawake 49,188 na Wanaume 64,195) sawa na asilimia 88 ya waombaji kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza.

**44.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa na uhitaji. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi 652,763,079,647.00** kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa wanufaika 202,877 ambapo **Shilingi 652,176,491,647.00** zimetolewa kwa wanafunzi wanaosoma ndani ya nchi na **Shilingi 586,588,000.00** kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi.

**45.** Mheshimiwa Spika, vilevile kupitia SAMIA Scholarship, Serikali imetoa ufadhili wa **Shilingi 2,754,370,430.00** kwa wanafunzi 593 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi katika kidato cha 6 ambao wanaendelea kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Afya na Sayansi Shirikishi (Science, Technology, Engineering, Mathematics or Health and Allied Sciences) katika ngazi ya Shahada.

**46.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau katika kutoa mikopo ya elimu kwa wanafunzi ambapo Benki ya NMB imezindua huduma hiyo kwa wanafunzi kupitia mzazi au mlezi. Katika mwaka 2022/23 **Shilingi bilioni 200** zimetengwa na mkopaji anaweza kukopa kuanzia **Shilingi 200,000.00** hadi **Shilingi 10,000,000.00** kwa marejesho ya riba nafuu ya **asilimia 9.**

**47.** Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuushukuru uongozi wa Benki ya NMB na natoa rai kwa taasisi nyingine za kifedha pamoja na wadau mbalimbali wa elimu nchini kuiunga mkono Serikali katika jitihada za kutoa mikopo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo ya elimu nchini.

**48.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wetu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya kikanda na kimataifa. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 76 wa Kitanzania katika nchi ya Uingereza (Jumuiya ya Madola) wanafunzi watatu, Hangaria 21 na China 52 katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamivu; na

(ii) imewezesha mafunzo kwa vitendo katika kilimo kwa wanafunzi 250 nchini Israel kwa kipindi cha miezi 11 kwa lengo la kujifunza kwa vitendo masuala ya kilimo katika nchi hiyo.

**49.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na utendaji kazi. Katika kufikia azma hiyo Serikali, imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo ya kuandaa mitaala kwa wahadhiri 280 wa Vyuo Vikuu ili kuandaa mitaala kwa kuzingatia miongozo, viwango na mahitaji ya sasa; na

(ii) imewezesha mafunzo kwa wahadhiri na watumishi 2,127 (wahadhiri 192 kuhusu namna bora ya ufundishaji, watumishi 845 mafunzo ya muda mrefu na na watumishi 1,090 muda mfupi) katika Taasisi za Elimu ya Juu.

**50.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kuongeza fursa za mafunzo katika Taasisi za Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo mtambuka lenye maabara nane na vyumba 11 vya maandalizi, ofisi saba, madarasa nane na stoo saba katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Aidha, imeanza taratibu za kupata hati miliki kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya chuo hicho katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoa wa Ruvuma; na

(ii) imekamilisha ukarabati wa vyumba vya madarasa 30, mabweni mawili, maabara, ofisi saba, nyumba 10 na miundombinu ya TEHAMA katika Chuo Kikuu Ardhi.

**g. Kuimarisha Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Maendeleo ya Taifa**

**51.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu nchini kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa wabunifu wachanga 83 na rasilimali fedha kwa wabunifu 27 walioibuliwa katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) mwaka 2022 kwa lengo la kuendeleza bunifu na teknolojia ili zifikie hatua ya ubiasharishaji; na

(ii) imetambua teknolojia mpya 27 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa nchini hadi sasa kufikia 506. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa kwa ajili ya rejea kuhusu taarifa za teknolojia na ubunifu zinazozalishwa nchini.

**52.** Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeendelea kubidhaisha teknolojia na ubunifu kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kuongeza ufanisi katika kuchangia maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendeleza ubunifu wa Prepaid Water Meter kwa kutengeneza na kufunga mita 20 kwa majaribio katika Wilaya 10 za mikoa mitano ambapo kila Wilaya ilipata mita mbili kama ifuatavyo: Tanga (Handeni na Pangani), Morogoro (Morogoro Vijijini na Mvomero), Pwani (Bagamoyo na Mkuranga), Iringa (Iringa Vijijini na Mufindi), na Njombe (Makete na Wanging'ombe). Ubunifu huo utawezesha udhibiti wa matumizi ya maji na ukusanyaji wa mapato; na

(ii) imewezesha kampuni changa mbili za Teknolojia na Ubunifu ambao ni **'Smart Darasa** na **Dawa Mkononi'** kushiriki katika shindano la ubunifu ambalo lilifanyika nchini Afrika Kusini lenye lengo la kuendeleza ubunifu. Aidha, shindano hilo lilishirikisha waanzilishi 13 kutoka Namibia, Afrika Kusini, Botswana na Zambia ambapo ubunifu wa '**Dawa Mkononi'** kutoka Tanzania uliibuka mshindi wa pili.

**53.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya mionzi ya nyuklia nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imepima sampuli 21,583 za vyakula, mbolea, tumbaku na bidhaa nyingine kati ya 28,000 zilizolengwa kupimwa kutoka mipakani, viwanja vya ndege na bandari ambapo kipimo kilionesha kuwa hakuna uchafuzi wa mionzi;

(ii) imekagua vituo 184 vyenye vyanzo vya mionzi ambapo vituo 168 vilikuwa katika hifadhidata na vituo vipya 16 kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa usalama kwa watumiaji; na

(iii) imetoa jumla ya leseni 314 ambapo leseni 220 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi, 62 za uingizaji (import); saba za kupeleka nje ya nchi (export); na leseni 25 kwa ajili ya usafirishaji wa mionzi.

**h. Kuimarisha na Kuendeleza Tafiti na Matumizi ya Matokeo yake katika Ajenda ya Maendeleo**

**54.** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa utafiti na matumizi yake katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii na kuchangia maendeleo ya nchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa kufanya utafiti na kutumia matokeo ya utafiti kwa kutoa machapisho 1,836 kupitia Taasisi za Elimu ya Juu katika majarida ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuchangia katika kuvitangaza (Visibility) Vyuo hivyo.

**55.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuanzisha, kuratibu na kusimamia miradi mbalimbali ya utafiti na ubunifu katika taasisi za Elimu ya Juu na Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuongeza maarifa na kutatua changamoto katika jamii. Azma hiyo imefikiwa kwa kufanya miradi ya utafiti 418 katika Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu Vishiriki na Taasisi za Utafiti na Maendeleo.

**56.** Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha wataalamu kuandika na kuchapisha kazi za utafiti, Serikali imeandaa Mwongozo wa Utoaji Tuzo kwa Watafiti watakao chapisha utafiti wao katika Majarida yenye hadhi ya Kimataifa 'High Impact Factor Jounals' katika Fani za Sayansi Asilia na Tiba.

**D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**57.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa washiriki 23 kutoka vyombo vya habari, wawakilishi wa Serikali kutoka Idara ya Habari Maelezo na wanachuo kutoka chuo Kikuu cha SUZA kuhusu nafasi ya vyombo vya habari katika kukuza utawala wa haki na sheria;

(ii) imeratibu mafunzo dhidi ya mapambano ya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu na mbinu haramu michezoni kwa kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo washiriki 230 wakiwemo wakufunzi, viongozi wa michezo, wanamichezo na watunga sera walishiriki; na

(iii) imeendelea kufanya utambuzi wa Taasisi zinazokidhi vigezo vya kujiunga na Mitandao ya Elimu ya UNESCO. Vilevile, imehuisha mikataba minne inayohusiana na Elimu ya Juu.

**Tanbihi: TAARIFA YA KINA YA UTEKELEZAJI YA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KINA INAPATIKA KATIKA KITABU CHA HOTUBA UK. 6 - 51**

**E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**58.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vitano vyenye lengo la kuongeza ubora wa elimu, kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata maarifa, ujuzi, kujiamini, kujiajiri na kuajirika.

**59.** Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni kama vifuatavyo:

(i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu na kuanza utekelezaji;

(ii) Kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika elimu ya sekondari na Vyuo vya Mafunzo ya Amali;

(iii) Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari;

(iv) Kuongeza fursa na ubora wa Elimu ya Juu; na

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**a. Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu**

**60.** Mheshimiwa Spika, Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu pamoja na kuanza utekelezaji wake ili kuimarisha maarifa na ujuzi kwa wahitimu wa ngazi zote za elimu. Aidha, Serikali itafanya mapitio ya sheria ya elimu na sheria mbalimbali za Taasisi za Elimu ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

**b. Kuongeza Fursa na Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) kwa Sekondari na Vyuo vya Kati vya Amali**

**61.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) kwa shule za sekondari na vyuo vya ualimu kwa itawezesha ukarabati wa shule za sekondari za ufundi na kuzipatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Aidha, itaboresha vyuo vya ualimu 10 kwa kujenga karakana na kuweka mitambo na vifaa katika vyuo hivyo ambavyo ni: Kitangali, Ndala, Nachingwea, Kleruu, Mtwara (U), Mpwapwa, Korogwe, Dakawa, Bunda na Kabanga kwa lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi kwa vitendo.

**62.** Mheshimiwa Spika, vilevile, Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara ufundi vitawezesha walimu tarajali kupata mafunzo ya Shahada ya Amali kwa kutumia wahitimu wa Vyuo vya Ufundi (TET) na Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET).

**63.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za elimu ya amali kwa kuendelea kusajili na kudahili wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya amali. Aidha, katika kuongeza idadi ya walimu wa ufundi, Serikali itadahili wanafunzi 660 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro – MVTTC.

**64.** Mheshimiwa Spika, katika kuwajengea umahiri walimu wa vyuo vya mafunzo ya amali na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuinua ubora wa mafunzo, Serikali itatoa mafunzo kwa wakufunzi 1,450 kuhusu ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri (CBET) kwa lengo la kuwa na walimu mahiri watakaotoa mafunzo kwa wanachuo ili waweze kujiajiri na kuajirika.

**65.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 64 katika Wilaya ambazo hazina vyuo hivyo pamoja na ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Songwe na itaanza kutoa mafunzo ya amali katika vyuo 29 vilivyokamilika. Vilevile, itakamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma ambapo kukamilika kwa awamu hiyo kutawezesha kudahili wanafunzi 1,500.

**c. Kuwezesha Ongezeko la Fursa na Ubora wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**66.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za Elimu kwa kutoa ithibati kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kusajili shule za msingi na sekondari takribani 560. Aidha, itaanza kusajili shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa mfumo wa kieletroniki.

**67.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kununua na kusambaza zana na vifaa saidizi kwa walimu tarajali, walimu na wakufunzi wenye mahitaji maalum.

**68.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kubaini na kukuza vipaji vya uandishi unaozingatia ubunifu kwa lengo la kujenga tabia ya kujisomea, kuhifadhi historia, mila na desturi za jamii pamoja na kuimarisha vipaji vya sanaa na michezo. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itasimamia utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yenye lengo la kuwatambua na kuwazawadia waandishi mahiri katika nyanja ya riwaya, hadithi fupi na ushairi kwa lengo la kukuza kazi

za uandishi bunifu, uchapaji na kuongeza idadi ya machapisho katika shule na maktaba nchini; na

(ii) itaendelea kuratibu mashindano ya uandishi wa insha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ili kukuza stadi za uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini.

**69.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uthibiti ubora wa elimu kwa ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule kwa kufanya ugatuaji kutoka ngazi ya kanda kwenda ngazi ya mikoa ili kusogeza huduma karibu na wadau na kuzifikia asasi nyingi; na

(ii) itafanya tathmini ya jumla ya shule na asasi 6,700 katika maeneo yafuatayo: mafanikio ya wanafunzi; ubora wa ufundishaji kwa ujifunzaji na upimaji; ubora wa uongozi na utawala; ubora na mazingira ya shule na matokeo yake katika ustawi, na afya na usalama wa wanafunzi na ushiriki wa jamii. Vilevile, itanunua magari 12 na kuweka samani katika ofisi 195 za uthibiti ubora wa shule kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji wa kazi.

**70.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ujifunzaji na kuongeza ufaulu wa wanafunzi, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha katika shule za msingi, sekondari pamoja na wathibiti ubora wa shule kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu 10,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati wa shule za sekondari Kidato cha 1 – 4; mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 4,500 wa shule za sekondari 1,300; mafunzo kuhusu programu ya shule salama kwa wakuu wa shule za Sekondari na Wathibiti Ubora wa Shule 1,378; mafunzo kuhusu unasihi na ulinzi wa mtoto kwa walimu 3,370 wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu; mafunzo kuhusu ufundishaji wa moduli za masomo 18 hatua ya I na II kwa walimu 600 kutoka katika vituo 151 vya Elimu kwa Njia Mbadala kwa lengo la kuongeza umahiri na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji; na

(ii) itaendelea kuwajengea uwezo walimu 12,000 wa shule za msingi katika upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika mikoa 10 iliyokuwa na wastani wa chini wa stadi hizo.

**71.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali, Darasa la I na III, Sekondari Kidato cha 1 na Elimu ya Ualimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na vitabu vya nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wasioona.

**72.** Mheshimiwa Spika, katika kuongeza idadi ya vitabu vya ziada na rejea vitakavyosaidia walimu na wanafunzi kukuza uelewa wa mada mbalimbali, Serikali itatathmini vitabu vya ziada na rejea kutoka kwa waandishi binafsi. Aidha, itawezesha uchapaji wa vitabu vya viongozi mbalimbali wa Kitaifa kwa lengo la kukuza uzalendo na maarifa kwa wanafunzi. Vitabu hivyo ni pamoja na: Maisha ya Benjamin William Mkapa; Kitabu cha Maisha ya Ali Hassan Mwinyi; Kitabu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; na 38 Reflections on Mwalimu Nyerere.

**73.** Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu, Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa vyumba 90 vya madarasa, matundu ya vyoo 360, mabweni 10 ya wasichana, nyumba 38 za walimu na maabara 20 za sayansi. Vilevile, itawezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 10 za wanafunzi wenye mahitaji maalum kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania; na

(ii) itakarabati miundombinu ya maabara za kilimo, sayansi, lugha na sayansi kimu katika Vyuo vya Ualimu saba ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo. Aidha, itaendelea kuunganisha vyuo vya ualimu 11 katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**74.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la maktaba ya Taifa Makao Makuu Dodoma ambalo pia litatumika kuhifadhi nyaraka na machapisho kwa lengo la kutunza historia, maarifa, maadili, na mila na desturi za Mtanzania. Vilevile, itajenga maktaba ya Mkoa wa Singida ambayo itawezesha upatikanaji wa huduma za maktaba.

**75.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukuza na kuendeleza kisomo na elimu kwa umma kwa kuanzisha madarasa 1,000 ya kisomo yanayolenga kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Watu Wazima. Aidha, itaendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea ujuzi vijana 12,000 kupitia Mpango wa elimu changamani kwa walio nje ya shule awamu ya pili (IPOSA).

**76.** Mheshimiwa Spika, katika kuboresha uongozi na usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu itatoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa walimu wakuu 6,500 wa shule za msingi.

**77.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania itaendesha Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa wanafunzi 1,815,792, Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,537,171, Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa wanafunzi 691,078, Kidato cha Nne kwa watahiniwa 610,330 na mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 8,500, Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 94,920 na Mtihani wa ngazi ya Cheti na Stashada ya Ualimu kwa watahiniwa 8,505.

d. **Kuongeza Fursa na Ubora wa Elimu ya Juu**

**78.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaratibu na kuongeza fursa za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itadahili wanafunzi 135,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vya Elimu ya Juu kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Awali na Umahiri;

(ii) itatoa nafasi 100 za ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali nje ya bara la Afrika kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu;

(iii) itaongeza fursa za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka 202,877 hadi 210,169; na

(iv) itaendelea kutoa fursa za Elimu ya Juu kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kutoka wanafunzi 593 hadi 1200 kupitia Samia Skolashipu.

**79.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaboresha mafunzo ya udaktari na kuongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ikiwemo shule ya meno na kuendelea na mradi wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia, utafiti na kutoa huduma za tiba kwa jamii. Vilevile, itaimarisha miundombinu ya kufundishia katika kituo cha umahiri cha magonjwa ya moyo na mishipa ya damu kampasi ya Mloganzila.

**80.** Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi katika taasisi za Elimu ya Juu nchini, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa Wanataaluma na Wataalam 1,197 wa Elimu ya Juu.

**81.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya Taasisi za Vyuo Vikuu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga kampasi 14 za Vyuo Vikuu katika mikoa ambayo haina kwa lengo la kuandaa rasilimaliwatu wenye ujuzi watakaowezesha kuleta mageuzi ya kiuchumi. Vilevile, itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Taasisi za Elimu ya Juu.

e. **Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

**82.** Mheshimiwa Spika, katika kuongeza maarifa na kutatua changamoto mbalimbali katika jamii Serikali itafanya utafiti katika maeneo 177 ya elimu, lugha, kilimo, biashara, uvuvi, mifugo, tiba, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano, maliasili, sayansi, teknolojia, watu wenye mahitaji maalum, kilimo na chakula, uongozi na biashara. Vilevile, itaendelea kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu katika nyanja mbalimbali. Aidha, itaandaa machapisho 1,806 kwa lengo la kueneza matokeo ya utafiti kwa jamii.

**83.** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwatambua wabunifu, kuwaendeleza na kubiasharisha ubunifu wao pamoja na kuendeleza miradi mbalimbali ya ubunifu kwa lengo la kukuza utaalamu asilia kwa kuendeleza teknolojia zinazozalishwa na wabunifu nchini.

**84.** Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na jamii. Aidha, itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye vyanzo vya mionzi. Vilevile, itafuatilia hali ya usalama wa hewa katika anga kupitia vituo 1,045.

**F. TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**85.** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, itaendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa ya UNESCO. Vilevile, itatoa elimu kwa Taasisi na Mamlaka za Serikali kuhusu Mkataba wa 2001 wa Urithi wa Chini ya Bahari (Underwater Heritage) ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo mbioni kuuridhia. Aidha, itafuatilia na kutathmini maeneo mapya ya urithi yaliyopendekezwa na wadau ili kuongeza maeneo zaidi ya urithi wa dunia nchini yanayotambuliwa na UNESCO kwa lengo la kuongeza vivutio vya utalii.

**G. SHUKRANI**

**86.** Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa QS Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Franklin Jasson Rwezimula kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, bila kuwasahau Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuwezesha kuandaliwa kwa hotuba hii.

**87.** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru pia Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi, na Wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wamiliki na Mameneja wa Shule, Vyuo na Taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu nchini.

**88.** Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru Washirika wa Maendeleo na Wadau wote wa Elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali ya Misri, Msumbiji, Morocco, Namibia, Tunisia, Mauritius, Comoro, Ethiopia, Zimbabwe, Algeria, Afrika Kusini, Malawi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Malaysia, Netherland, New Zealand, Norway, Palestina, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**89.** Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, Global Partnership in Education (GPE), United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF), United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), United States Agency for International Development (USAID), Benki ya Dunia, Inter University Council for East Africa (IUCEA), Human Development Innovation Fund (HDIF), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, Aga Khan Education Services, Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Water Aid, Plan International, Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Mo Foundation, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na Christian Social Services Commission (CSSC).

**H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24**

**90.** Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,675,753,327,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 537,880,762,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 500,957,569,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 36,923,193,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 1,137,872,565,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 979,083,678,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 158,788,887,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**91.** Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,733,888,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 1,124,980,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,608,908,000.00).**

**92.** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Fungu 46 na Fungu 18 yenye jumla ya **Shilingi 1,678,487,215,000.00.**

**93.** Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**94.** Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara http://www.moe.go.tz.

**95.** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**Tanbihi: TAARIFA YA KINA KUHUSU MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 INAPATIKA KATIKA KITABU CHA HOTUBA UK. 52 - 88**

MAWIO YA MEMBE

# Anabakia kuwa mkosoaji wa Rais, Mwenyekiti wa chama chake 'live'

• Alifikirisha wengi pale alipoamua jambo lake



Bernard Membe aliporudishiwa kadi ya CCM Mei 29,2022. Kushoto ni aliyekuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa, Shaka Hamdu Shaka, akiwa kijijini Chiponda Rondo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JUA lilipochomoza Novemba mwaka 1953 mkoani Lindi, alizaliwa mwanadiplomasia Bernard Membe, ambaye ameondoka baada ya miaka 69 ya uhai wake, akitumia muda mwingi kuitumikia serikali na Watanzania.

Membe ambaye alipozaliwa katika Kijiji cha Chiponda-Rondo, hakuna aliyejua kuwa alikuwa na maono makubwa kwenye siasa, amekuwa Naibu na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika awamu ya Rais Jakaya Kikwete, kuanzia 2005 hadi 2015.

Amefariki Ijumaa Mei 12, muda mfupi baada ya kuugua 'nyumonia' kali na kulazwa katika hospitali ya Kairuki jijini Dar es Salaam. Kifo chake kimekuja kipindi kifupi baada ya kurejea CCM, akijiondoa tena ACT-Wazalendo, aliyojiunga nayo 2020 na kuwa mshauri mkuu wa chama na baadaye kuwa mgombea urais kupitia chama hicho akipambana na mgombea wa CCM, John Magufuli.

Waziri Membe alisifika kwa upole, akizungumza au kuongea kwa sauti ya utulivu, yenye unyenyekevu na muda wote, alikuwa akitabasamu na kuwasiliana na kila mmoja awe mzee au kijana kwa taratibu na utaratibu.

Ni jambo linalodhihirisha kuwa hakuwa au hakupenda kufoka wala kukemea, lakini akifanya kila kitu katika utumishi wa umma kwa kuheshimu, kuthamini na kushirikiana na kila mmoja, huku akisikiliza kwa moyo kila aliyewasiliana naye.

> Baada ya kutimuliwa Februari 2020, hakuwa na papara ila alinyamaza kwa miezi kadhaa na ilipofika Julai alitoa ya moyoni japo hakumaliza kila kitu.

Anastahili sifa kwa kulitumikia taifa kwa heshima kuu, lakini pia kuwa mwanadiplomasia aliyeishi muda mrefu katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi.

Mwanadiplomasia huyu ni msomi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Johns Hopkins University huko Marekani, hatasahaulika na wapigakura wake wanajimbo lake la Mtama mkoani Lindi, aliowatumika kwa miaka 10.

## MWANADIPLOMASIA WA AFRIKA

Waziri wa zamani Membe ameacha alama Afrika hasa kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya Maziwa Makuu mathalani ule wa DRC, ni juhudi ambazo hazitasahaulika barani humo.

Aliamini kuwa DRC mzozo wake, siyo tu kuwa una vipimo na athari za kikanda na kuvuka mipaka, lakini pia ulihitaji juhudi za kikanda katika kuutatua kwa njia endelevu na za kidiplomasia.

Katika uhai wake aliamini na kufanyakazi usiku na mchana kupata suluhu ya mgogoro wa DRC akisema ni taifa linalopakana na nchi tisa za Afrika za Angola, Burundi, Rwanda, Uganda, Jamhuri ya Congo, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Sudan Kusini, Tanzania na Zambia.

Katika juhudi zake alifanyakazi kubwa kumaliza mizozo ya Maziwa Makuu na wa DRC, hasa akisema kukosekana utulivu , kuna hatari nyingi kwa nchi jirani na ukanda mzima wa kusini, mashariki na hata Afrika ya Kati na kungeleta matokeo mabaya kwa watu kuishi katika migogoro isiyokwisha.

## HAKUWA MWOGA

Wakati wa uongozi wa Magufuli Membe hakutaka kukaa kimya na kuzibwa mdomo, licha ya kuwa mwana CCM kindakindaki na pia shushushu, alikuwa akitoa sauti ya kukosoa serikali ya JPM jambo lililokatisha uanachama wake ndani ya chama hicho.

Alikuwa hana hofu na kile alichokizungumza na wakati mwingine alizungumza na vyombo vya habari vya kimataifa, akisifia kazi ya JPM hata hivyo akikosoa na kueleza kuwa kuna baadhi ya mambo yalipaswa kurekebishwa.

Historia ndani ya CCM, inaonyesha kuwa Februari 2020, ulikuwa ni mwanzo mgumu kwa Membe ndani ya chama kilichomlea, kumkuza na kufanikisha kung'ara kwa nyota yake kitaifa na kimataifa.

Mwaka unaanza kwa kukabiliana uso kwa uso na chama chake -CCM ambacho kilimfukuza uanachama. Ni maamuzi ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, iliyokuwa chini ya Mwenyekiti John Magufuli, iliyomuweka pembeni, akidaiwa kuwa ni kutokana na matendo yake yasiyokuwa na maadili.

Ilipotimu Mei 29, 2022 mwaka mmoja uliopita, mgombea urais wa ACT Wazalendo, Bernard Membe alirudishiwa kadi yake ya uanachama wa CCM, baada ya kufukuzwa.

Baada ya kutimuliwa Februari 2020, hakuwa na papara ila alinyamaza kwa miezi kadhaa na ilipofika Julai alitoa ya moyoni japo hakumaliza kila kitu.

Ni pale Membe anapotangaza rasmi mbele ya jamaa zake wakazi wa nyumbani kwao huko kijijini Rondo, kuwa atagombea urais katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020.

Hata hivyo, aliwaachia maswali mengi , hakutangaza wazi wazi kuwa atagombea kupitia chama gani ila wapo waliokuwa wanaeleza kuwa atajiunga na chama cha ACT Wazalendo, kwa kuwa CHADEMA tayari Tundu Lissu, alikuwa ameshaweka wazi msimamo wake kuwa anapambana na Magufuli kuwania uongozi wa Tanzania.

Kwa ujumla alikuwa ngangari na asiyeogopa kuvunjwa mwiko. Japo si vibaya kwa mujibu wa katiba ya CCM lakini ni kama Membe alitaka kwenda kinyume na mazoea kwa kuanzisha upinzani wa ndani ya chama kwenye kugombea urais wakati chama kimeweka mazingira ya aliyekuwapo madarakani kugombea bila kupingwa kwenye muhula wa pili wa miaka mitano ya kumalizia ngwe ya uongozi wake.

Baada ya uchaguzi, alibaki kimya hadi aliporudishwa tena ndani ya CCM na Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa wakati huo, Shaka Hamdu Shaka, aliyefika nyumbani kwao katika Kijiji cha Chiponda- Rondo kumpokea tena.

Mwenezi wa CCM Shaka, alisema anarudishwa kundini baada ya Membe kuomba msamaha, lakini naye hakufanya ajizi akijibu kuwa hakuwa tena na sababu za kumzuia kuwa mwanachama wa CCM, bila kufafanua kwa kina.

Lakini ujumbe ukafika na kila mmoja akaelewa kama alivyojaliwa na ufahamu wake, kwa vile wengi walihusisha kutimuliwa kwake na kuonyesha nia ya kugombea urais, wakati wa uongozi wa Rais JPM, akimaanisha kuchuana na mwanaCCM aliye madarakani.

Kutikiswa kwa Membe kwenye siasa kunakohusishwa na kukosa maadili hadi kufa kwake hakukueleza bayana ni makosa gani ambayo anatuhumiwa kuyafanya , wakati huo akituhumiwa pamoja na makada ambao ni pamoja na makatibu wakuu wastaafu, Yusufu Makamba na Abdulrahman Kinana.

Hayati Membe aliyezikwa jana kijijini kwake, alizaliwa Novemba 9, 1953 na taratibu baada ya miaka kadhaa ya utumishi aling'ara zaidi kuanzia 2005, aliposhinda kiti cha ubunge wa jimbo la Mtama.



## Ujenzi wa maabara ya kisasa Dodoma washika kasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) linaendelea na ujenzi wa maabara ya kisasa Dodoma itakayorahisisha upatikanaji wa majibu ya haraka ya sampuli za watumiaji wa mikoa ya kanda ya kati.

Mwenyekiti wa Bodi ya TBS, Prof. Othman Chande Othman, akizungumza jana baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa maabara hiyo unaokwenda sambamba na ujenzi wa ofisi za TBS jijini Dodoma, alisema kukamilika kwa maabara hiyo itaongeza ufanisi na kusaidia watumiaji wa maabara kupata sampuli zao kwa haraka.

Alisema mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi na maabara ya kisasa ya TBS Dodoma unatarajia kugharimu Sh. bilioni 25 na unatarajia kukamilika ifikapo Machi mwakani.

Mwenyekiti huyo alisema hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 35 na baada ya kukagua ameridhishwa na kasi ya ujenzi huo.

"Maabara hii inayojengwa itakuwa ya kisasa ambayo itahudumia wananchi wa Mkoa wa Dodoma na mikoa ya jirani. Pia tunatarajia majibu ya sampuli ambayo yatatolewa yatakuwa ni ya ubora wa juu ndani na nje ya nchi na itaongeza utendaji kasi wa shirika kwa asilimia 50," alisema.

Alibainisha kuwa kukamilika kwa maabara hiyo pia kutapunguza mzigo kwa maabara kuu ya mkoani Dar es Salaam lakini pia itapunguzia wananchi gharama za kufuata huduma.

Prof. Othman alisema maabara hiyo itafungwa teknolojia za kisasa ambazo zitawasiliana na maabara zingine kwenye uchunguzi na vipimo lakini utakuwa na teknolojia ya kupima bidhaa za kielektroniki.

# Dk. Gwajima: Wazazi walindeni watoto dhidi ya ukatili kijinsia

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi kujenga tabia ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo kwa asilimia 60 vinatokea ndani ya nyumba zao.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia iliyofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini hapa.

Alisema kutokana na kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini wazazi wanapaswa kuwalinda watoto wao kuliko hata wanavyolinda mali zao.

"Wazazi lazima tubadilike ili kulinda watoto wetu kuliko tunavyolinda mali zetu leo hii wazazi wamekuwa wepesi sana kulinda nyumba, shamba unakuta mbuzi akiibiwa kwa mjumbe hakukaliki lakini watoto wetu hatuwalindi matokeo yake unakuta mtoto kafanyiwa vitendo vya ulawiti sisi hatuna hata habari," alisema Dk. Gwajima.

Kadhalika, alisema wazazi wanaowajibu huo kutokana na vitendo hivyo kwa asilimia kubwa kutokea ndani ya nyumba zao na kufanywa na watu wa karibu wa familia.

"Kwenye aibu yetu ndipo shetani alipojificha mzazi unajifanya wewe unahuruma umekaribisha ndugu zako lakini hao ndiyo wanakuwa wa kwanza kuharibu watoto wako sisemi kuwa mkawafukuze lakini mnapaswa kulinda watoto wenu kuliko mnavyolinda mali zenu," alisema Dk. Gwajima.

Pia alisema moja ya sababu ya kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini ni mmomonyoko wa maadili, kuiga mila na desturi za mataifa mengine.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq, alisema wamekutana katika siku hiyo ya kimataifa ya familia kujadiliana nini kifanyike na kipi kisifanyike ili kuimarisha familia.

Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Dk. Ezekieli Kyogo, alisema kama familia zitakuwa sawa mzigo wa matukio ya uhalifu yatapungua nchini.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mragili, alisema matukio ya unyanyasaji wa kijinsia katika Mkoa wa Singida yameendelea kushika kasi na ndani ya miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi 2023 matukio 842 yameripotiwa.

Akizungumza kwenye kongamano la Siku ya Familia kimkoa lililofanyika mkoani Singida, Mragili alisema kwa mujibu wa taarifa ya makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji kutoka Jeshi la Polisi matukio yaliyotokea katika kipindi cha mwaka 2022 yalikuwa 12,163 nchi nzima ambapo kati ya hayo kwa Mkoa wa Singida yalikuwa 325.

Serukamba alisema tatizo kubwa katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia inaanzia kwenye ngazi ya familia na wanafamilia wamekuwa chanzo cha ukatili baina ya mke na mume, baba kwa mtoto au walezi kwa mtoto.

**Imeandaliwa na Paul Mabeja (Dodoma), Thobias Mwanakatwe (Singida).**




Mkuu wa Magereza Msaidizi na Mganga wa Zahanati ya Gereza la Msalato, SP Dk. Abusalum Mpamba (kushoto), akipokea msaada wa dawa kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Sonia Mkumbwa kwa ajili ya zahanati hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TMA yawaonya wanaotoa taarifa hali ya hewa kiholela

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dk. Ladislaus Chang'a, amewaonya wamiliki wa vituo vya hali ya hewa nchini kuacha tabia ya kutoa taarifa zao holela kwa kuwa ni kinyume na sheria.

Alitoa onyo hilo jana baada ya kufungua semina ya siku moja kwa ajili ya kujadili mapungufu yaliyopo katika mamlaka hiyo na kuyafanyia maboresho ili kufikia viwango vya kimataifa katika utoaji wa takwimu sahihi za hali ya hewa zitakazosaidia kuchochea maendeleo ya nchi.

Alisema Sheria Namba 2 ya Mwaka 2019 ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inakataza mtu yeyote kusambaza taarifa za hali ya hewa bila ya kuwa na kibali.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuzitumia taarifa zinazotolewa na vyanzo rasmi ikiwamo mamlaka hiyo ya TMA, katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

Vile vile aliwataka wamiliki wote wa vituo vya hali ya hewa nchini kuvisajili kwa mamlaka husika ili vitambulike badala ya kuendelea kutoa huduma pasipo usajili wowote hali ambayo ni kinyume na sheria za nchi.

Pia aliipongeza serikali kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya TMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa takwimu zenye usahihi ili kufikia viwango vya kimataifa kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

Naye mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo (UNDP), Alfrei Maseke, alisema semina hiyo inalenga kuiwezesha Tanzania katika kuboresha miundombinu ya hali ya hewa na kuongeza ufanisi wa taarifa zinazotolewa na TMA ili kuwa na tija katika jamii.

Alisema: "Semina hii inatokana na Mfuko wa Uboreshaji wa Ufuatiliaji taarifa za Hali ya Hewa (SOFF) na Tanzania ni moja kati ya nchi 26 duniani zitakazonufaika na mpango huu ambao lengo lake ni kuimarisha miundombinu ya hali ya hewa pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu".





# Watakaobainika kutorosha tumbaku kufikishwa mahakamani

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewatahadharisha wakulima na wanunuzi wa tumbaku wilayani Chunya watakaodiriki kutorosha zao hilo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa tahadhari hiyo juzi kupitia hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon Mayeka kwenye kikao cha wadau wa tumbaku kilichokuwa na lengo la kufanya tathmini ya uzalishaji wa zao hilo.

Kikao hicho kiliitishwa na Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wilayani humo (CHUTCU) na kuwashirikisha wadau mbalimbali wa kilimo zikiwamo taasisi za kifedha, wakulima, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na maofisa wa kampuni zinazonunua zao hilo.

Alisema mbali na kuwafikisha mahakamani watakaokamatwa, pia tumbaku hiyo itataifishwa pamoja na chombo kitakachokutwa kinatumika kwenye usafirishaji huo.

Alizitaka kampuni zinazonunua tumbaku kwa wakulima kuwalipa fedha zao kulingana na madaraja na kwamba lazima ziwalipe mapema ili wafanye maandalizi ya msimu mwingine.

"Kampuni zinatakiwa kununua tumbaku ya wakulima kwa bei nzuri kulingana na madaraja, lakini zikishanunua ni marufuku mtu yeyote kutorosha tumbaku, ni lazima biashara ifanyike kwenye mfumo wa ushirika," alisema Mayeka.

Katika hatua nyingine Mayeka aliwataka wakulima wilayani humo kujiunga na bima za mazao ili wafidiwe endapo mazao yao yatakumbwa na majanga mbalimbali ikiwamo mvua ya mawe na ukame ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Meneja Mkuu wa CHUTCU, Christian Msigwa, alisema katika msimu wa kilimo uliopita baadhi ya wakulima walikuwa wanachanganya tumbaku na wengine walikuwa wanamwagilia maji ili kuongeza uzito jambo ambalo lilikuwa linaharibu soko.

Alisema wakulima wengine walikuwa wanachelewa kuuza tumbaku zao hali ambayo ilikuwa inasababisha zikauke zaidi na kupungua uzito na hivyo kuwalazimu kuanza kufanya uhuni kwa kuchanganya ili kuongeza uzito.

Alisema ili kukabiliana na matatizo hayo walitoa elimu kwa viongozi wa vyama vyote vya msingi vya wakulima 21 vilivyopo ili wawashauri wakulima wao kuacha kuchanganya majani ya tumbaku.

Mrajisi wa vyama vya ushirika mkoa wa Mbeya, Peter Zengo, alisema Bodi ya Tumbaku (TTB), itatoa mwongozo kuhusu upatikanaji wa kampuni za ununuzi wa tumbaku ili kuepusha migongano ambayo haina sababu.

Alisema msimu ujao wa kilimo umeanza maandalizi ya kupata pembejeo mapema ili wakulima waanze mapema msimu na kuongeza uzalishaji.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wakulima kutafuta wadau wa kuboresha soko la zao hilo na kwamba kwa sasa soko limeanza kuboreka baada ya ongezeko la wanunuzi.

Aidha aliziomba kampuni zinazonunua tumbaku wilayani humo kushirikiana na vyama vya msingi vya wakulima wa tumbaku kujenga mabani ili kuboresha maandalizi ya tumbaku.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akikabidhi Sh. milioni 5 kwa viongozi wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Mbarali, ambayo ni sehemu ya Sh. milioni 10 alizotoa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# UWT yapewa mil.10/- utekelezaji miradi maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amekabidhi Sh. milioni 10 kwa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mahundi amekabidhi fedha hizo kwa awamu mbili tofauti ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya kutoa Sh. milioni 20 kwa UWT katika kila wilaya ili kuupunguzia umoja huo hali ya utegemezi.

Alikabidhi fedha hizo juzi kwenye kikao cha baraza la kikatiba la umoja huo Wilaya ya Mbarali kilichoambatana na mafunzo maalumu kuhusu masuala ya ujasiriamali na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya wilaya hiyo.

Alisema lengo lake ni kuifanya jumuiya hiyo kuwa na miradi ya kujiingizia kipato ili kuepuka kuwa tegemezi hasa wanapotekeleza shughuli zao.

Aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuendelea kushirikiana na kupendana ili kufikia malengo yao yakiwamo ya kushiriki kwenye uchaguzi kwa kuhakikisha wanashiriki vizuri kwenye uchaguzi na kupata wawakilishi.

Katika hatua nyingine aliwataka wanachama wa umoja huo kulipa ada za kila mwaka ili chama waendelee kupata mafanikio ikiwamo kutekeleza vizuri miradi.

Aliwataka kuendelea kumsemea vizuri Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Dk. Samia Suluhu Hassan, huku akiahidi kuungana nao baada ya kukamilika kwa vikao vya Bunge Julai mwaka huu.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi wilayani humo, Katibu wa UWT Wilaya ya Mbarali, Branca Mhagama, alisema kwa sasa wanatekeleza miradi miwili ikiwamo ujenzi wa nyumba ya kuishi ya katibu ambayo wameanza utekelezaji.

Alisema mbali na mradi huo pia wanaendelea na ujenzi wa vyumba vya maduka kwa ajili ya kupangisha na kwamba mradi huo ni miongoni mwa vitega uchumi ambavyo wanaendelea kujenga.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Mbarali, Zabibu Baharam, alimshukuru Naibu Waziri kwa mchango wake kwa maelezo kuwa utawasaidia kukamilisha baadhi ya maeneo yaliyobakia.

Alisema watahakikisha wanazitumia vizuri fedha hizo pamoja na za wadau wengine ili kuhakikisha wanaendelea kuaminiwa na kuendelea kuwasaidia kwenye miradi wanayotekeleza.

# TBS yawanoa wajasiriamali uzalishaji wa bidhaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS) limeanza kutoa mafunzo maalumu kwa wafanyabiashara, wajasiriamali na wasindikaji wa bidhaa mbalimbali ili kuwasaidia kuzalisha bidhaa zenye ubora ambao utakidhi ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi jijini Mbeya ambapo wadau mbalimbali walishiriki ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Viwango Afrika ambayo hufanyika kila mwaka ifikapo Oktoba 14.

Akifungua mafunzo hayo juzi, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alishukuru shirika hilo kwa kuanzisha mafunzo hayo akieleza kuwa yatawasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa ambazo zitakuwa na ubora unaokubalika katika soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema ili kuendelea kuboresha viwango vya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali, TBS inatakiwa kuweka maofisa wake mpaka katika ngazi ya kata ili wananchi wasogezewe zaidi huduma kwenye maeneo yao ya uzalishaji.

Alisema utaratibu huo unaweza ukawa na tija kama ambavyo Wizara ya Kilimo imefanya kwa kuweka maofisa kilimo katika ngazi hiyo na kuleta matokeo chanya.

Meneja wa Viwango wa TBS kutoka makao makuu, Mhandisi Yona Afrika alisema mafunzo hayo yalikuwa yanawalenga wasindikaji wa mazao ya kilimo ili wajue umuhimu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Alisema utaratibu huo utawasaidia kuzalisha bidhaa zenye viwango ambavyo vitakuwa na ushindani na zitaaminika na watumiaji kutokana na kuwa na nembo ya ubora.

Alisema kazi ya kuandaa viwango vya bidhaa mbalimbali ni ya wadau mbalimbali wakiwamo wakulima ambao ndiyo kundi la kwanza kwenye mnyororo wa uzalishaji lakini kundi hilo lilikuwa linasahaulika.

Meneja wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonda, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuendelea kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya ubora yanayotolewa ili wazalishe bidhaa zenye ubora.

Alisema mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa kwa wazalishaji kwa sababu yanasaidia kulinda afya za watumiaji wa bidhaa hizo pamoja na kuendana na matakwa ya kisheria.





## Dk. Mwinyi aimwagia sifa China ushirikiano na Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameishukuru Serikali ya China kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa Tanzania ikiwamo Zanzibar kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo.

Alitoa shukurani hizo Ikulu, Zanzibar wakati wa utiaji saini wa mikataba ya miradi mitano ya ushirikiano kwenye sekta ya afya baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya China.

Katika hafla hiyo Dk. Mwinyi alisema, Zanzibar imenufaika na fursa nyingi za maendeleo kupitia misaada tofauti inayoletwa kutoka China hasa sekta za afya na elimu.

Alisema mikataba minne iliyosainiwa itajenga ushirikiano mwema baina ya maofisa wa afya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na China jambo alilolieleza ni ishara ya uhusiano mwema uliopo baina ya mataifa mawili hayo.

Dk. Mwinyi alieleza uhusiano wa China na Tanzania utakumbukwa zaidi kwa kuinufaisha Zanzibar kupitia sekta ya afya katika suala la kuimarisha miundombinu ya afya, vifaa tiba, dawa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wataalamu wa kada hiyo.

Aidha, Dk. Mwinyi alimpongeza balozi mdogo wa China aliyepo Zanzibar, Zhang Zhisheng, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kukuza ushirikiano uliopo baina ya nchi hizo mbili.

"Wenzetu China mmetusaidia sana hata tukieleza hatutomaliza, nimeshuhudia utiaji wa saini mikataba minne ya ushirikiano baina ya Zanzibar na China, kupitia sekta ya afya, miradi hii itaendelea kuimarisha ushirikiano wetu uliopo," alisema Dk. Mwinyi.

Rais wa Taasisi ya Ushirikiano baina ya Afrika na China, (CAPFA) Dk. Li Bin, ameeleza miradi hiyo itatatua maradhi sugu jamii hasa kinamama na kutoa fursa za miradi mbalimbali itakayonufaisha pande zote za ushirikiano wa nchi hizo na kuboresha huduma za sekta ya afya.

Dk. Li pia aliisifu Tanzania kwa ukaribu wa kihistoria baina yake na China alioueleza ni wa muda mrefu tangu uhai wa Mao Zedong na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, zaidi ya miaka 50 iliyopita.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na raia wenye ukarimu, upendo na ushirikiano, ambao ni kielelezo chema kwenye kukuza uhusiano uliopo baina yao na China.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mikataba waliyoisaini itagharimu Dola za Marekani 4,76,000 (Sh.bilioni 1.2).

Miradi iliyosainiwa ni pamoja na mradi wa ushirikiano wa hospitali baina ya China na Afrika, utafiti na udhibiti wa magonjwa ya kitropiki ikiwamo kichocho, uchunguzi wa saratani ya shingo ya mlango wa kizazi na kituo cha matibabu ya mama na mtoto pamoja na msaada wa vifaa tiba.

Aidha, hospitali zitakazonufaika na ushirikiano huo ni Hospitali Kuu, Mnazi Mmoja, Kivunge, Chakechake na Abdallah Mzee Pemba.

# Serikali yakemea mikokoteni ya punda kuingia mjini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Masoud Muhammed, amesema tabia ya kuingiza magari ya ng'ombe na punda katika maeneo ya mjini yanachafua mandhari ya miji na kusababisha ajali barabarani.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana wakati akijibu swali la mwakilishi wa Tumbe, Said Saleh.

Waziri huyo alisema, SMZ inakiri kwamba hilo ni tatizo na kuona ipo haja kubwa ya kuendelea kufanya operesheni za mara kwa mara ili kukabiliana na baadhi ya wananchi wanaoifumbia macho adha hiyo.

"Jitihada za operesheni maalum ya usafi na kukamata magari ya ng'ombe na punda imefanyika na kufanikiwa kukamata magari yapatayo 17 katika maeneo ya Barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni na Amani –Mombasa, kwa ushirikiano na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mgharibi 'B' na Baraza la Manispaa Magharibi 'B' wahusika walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sharia," alisema.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo ng'ombe 15 walikamatwa katika maeneo ya Taveta, Melitano, Mbarali, Kijitoupele na Sokoni na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria husika.

Waziri huyo alisema serikali ina mikakati kwa ajili ya kutokomeza tatizo hilo ikiwamo kusimamia sheria zilizopo.

Alitaja mikakati mingine ni kufanya doria za mara kwa mara, kukamata magari ya ng'ombe na punda katika maeneo ya Manispaa na kuchukua hatua za kisheria kwa mujibu wa makosa yao.

Alisema watawataifisha wanyama wote na magari ya ng'ombe yanayokamatwa pamoja na kutozwa faini kwa mujibu wa taratibu za kisheria.



Mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake, Maisara Mjini Zanzibar jana, kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yawatoa hofu wananchi ujenzi wa barabara vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imejipanga kuhakikisha kwamba ahadi zote zilizotolewa na Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa wananchi zinatekelezwa ikiwamo za uimarishaji wa miundombinu ya barabara vijijini.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza la wawakilishi waliochangia makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Kassim alikuwa akijibu hoja za mwakilishi wa Ziwani Pemba, Suleiman Ali Makame, aliyetaka kujua kwa nini ahadi za Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa wananchi ikiwamo wapigakura wake hazitekelezwi.

Jamal alisema ahadi za Rais Dk. Mwinyi anazozitoa kwa wananchi zinatakiwa kutekelezwa kwa lengo la kujenga imani kwa wananchi pamoja na kuzipatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili.

Aidha mwakilishi wa Pandani (ACT-Wazalendo), Professa Omar Fakih Hamadi, alisikitishwa na serikali kushindwa kutimiza ahadi za Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa wananchi wake ambazo zimetolewa katika kipindi tofauti ikiwamo ujenzi wa barabara zinazokwenda vijijini.

Waziri Jamal alisema serikali ipo katika hatua za mwisho ujenzi wa barabara inayokwenda katika maeneo huru ya uchumi Micheweni Pemba ambayo itakapomalizika itakuwa kichocheo kwa wawekezaji kuwekeza miradi mikubwa ya maendeleo.

Alisema baadhi ya barabara ujenzi wake umesimama kufuatia mvua zinazoendelea za masika ambazo inakuwa vigumu kuendelea na harakati za ujenzi.

Aidha, alisema serikali inakusudia kuyafanyia ukarabati majengo ya Ikulu zake ikiwamo ya Mnazi Moja Unguja, Ikulu ya Pemba pamoja na Dar-es-Salaam ili ziwe na hadhi ya juu ya viongozi wa kitaifa.

Alisema baadhi ya majengo ya Ikulu hayajafanyiwa ukarabati wa muda mrefu, huku serikali ikiendelea na azma yake ya kujenga nyumba za viongozi wakuu wa kitaifa.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER PATRICK MARWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya TRAILER yenye namba za usajili T.973 DVP yenye Chassis No; SDCCS45300102903. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAH/TR/RB/321/2023.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA DODOMA**
**KANDA YA DODOMA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA.3 YA 2023**
**Maombi ya barua za usimamizi wa mirathi ya**
**ALEX JONATHAN**
**MWAISWAGA.........................................MAREHEMU**
**NA**
**1.REHEMA SAMSON MWAISWAGA............MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75 na 76)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi JUNI mwaka 2023.
Imetolewa leo tarehe 09 mwezi wa MEI,2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOM

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ROSE ANYWELWISYE MWABULESI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 269 CGD. Chassis No. L7GPCK7Y7K1015405. Engine No. KL157FMJ2K5015405. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/480812/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 50 YAMWAKA 2023**
**BAINA YA**
**GLORY LEONARD SHIRIMA ...............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KASSIM PASPHILY NKANA ........MDAIWA 1**
**FRANK MACHUMU ................ MDAIWA 2**
**FINI FINANCIALS & REAL ESTATE AGENCY SERVICES COMPANY LIMITED ............ MDAIWA 3**
**MBOGO AUCTION MART ............ MDAIWA 4**
**DAVID HESAU MWAKITWANGE .........MDAIWA 5**

**KWA;**
**KASSIM PASPHILY NKANA**
**FRANK MACHUMU**
**FINI FINANCIALS & REAL ESTATE AGENCY SERVICE COMPANY LTD**
**MBOGO AUCTION MART**
**DAVID HESAU MWAKITWANGE**

**POPOTE MLIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 25.05.2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 11 ya mwezi wa MEI, 2023.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ERIC E. OLOO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S.4827-0590** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. PETER CLAVER HIGH SCHOOL** mwaka **2019.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/165599/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SABRINA HAMISI SIMBA** anatangaza kupotelewa na Equivalence Certificate chenye namba **EQ2021004465** kilichotolewa na **HANA INTERNATIONAL SCHOOL UGANDA** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBD/RB/1840/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**REHEMA H. SHAO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba: **S5000/0532** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **WAMA-NAKAYAMA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2019.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/MAG/RB/163589/2023**

## KUPOTEA KWA NYARAKA ZA KANISA

**Askofu Ndugu Robinson Francis** wa Kanisa la **NCRCT (New Convenant Revival Church of Tanzania)** anatangaza kupotelewa na nyaraka zifuatazo za kanisa zilizokuwa chini ya uangalizi wa aliyekuwa Askofu **Jackson Majaliwa Leguna**; Cheti cha Usajili, Risiti za Ujenzi, Kitabu cha Kanuni, Hati, Katiba na Barua ya Umiliki. Vyote ni mali ya Kanisa. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/145544/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Morogoro**
**Kituo cha Mjini Mkoa Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi Na. 42/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU RASHIDI KISWANYA WA KONGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA**
**RASHIDI IDD KIMANGA**
**TANGAZO**
*Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za Usimamizi w a Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu , wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **1 mwezi 06 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia na Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa .
Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika
**Imetolewa tarehe 9 mwezi 05 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 43 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**KANUTI PAULO MZERU**

**By 1. MARTINA KAYEMBILI KANUTI**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be field on or before the **29 /05 /2023.**
Dated at **Morogoro**, this **15** day of **05, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI

KAMPUNI YA STELLE LODGE LIMITED YENYE NAMBA YA USAJILI 140446114 ILIYOKO MKOA WA ARUSHA KATA YA MLANGARINI BARABARA YA KISERIANI EAST AFRICAN KARIBU NA OFISI ZA RADIO FIVE INATANGAZA KUA IMEFUNGWA RASMI KUANZIA SASA.
WAKURUGENZI - WITNESS ROBERT SHUMA-TANZANIA
ALBERTO ARCANGELI- ITALIAN

Email:
shumawitness@gmail.com
Simu namba +255742707930,
P.O.Box 12439,
Arusha.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP.117,R.E.2002)**

By this deed I, **ALLY SALUMU HAMISI** an adults , **ISLAMIC** and resident of **LINDI** do solemnly state as follows:
1.That, I hereby absolutely renounce and abandon the use of former name of **ALLI SALUMU MAKATA** and in place thereof do assume and adopt the name of **ALLY SALUMU HAMISI**
2.That ,in pursuance of such change of name as aforesaid I do hereby declare that,I shall at all material times hereinafter in all records, deed and instruments in writing and in actions, proceedings and transactions and upon all occasion whatsoever use and sign the name of **ALLY SALUMU HAMISI** as the name in place of the former name of **ALLI SALUMU MAKATA**
3.That ,I further authorizes and request all people to designate and address me by such assumed name of **ALLY SALUMU HAMISI**
I make this declaration consciously believing the name to be in accordance with the provisions of Oaths and Statutory Act,1966.
Signed and Addressed by the **ALLY SALUMU HAMISI** this 8th day of **MAY** ,2023}

BEFORE ME:
NAME
SIGNATURE
ADDRESS:




**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# CENI yaanza ukaguzi daftari la wapiga kura

**KINSHASA,** DRC

TUME ya Taifa ya Uchaguzi Nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CENI) imeanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi wa daftari la wapigakura kwa kutumia maofisa wa taasisi za nje kuelekea uchaguzi wa Desemba mwaka huu.

**Tayari wanasiasa wa upinzani wakiongozwa na Moise Katumbi na Martin Fayulu wanapinga utaratibu ulioanzishwa na CENI...**

Inaelezwa kuwa mchakato wa kuwaandikisha wapigakura ulimalizika mwezi Aprili, licha ya kuwa sehemu kadhaa kama maeneo ya Rutshuru na Masisi mkowani Kivu kaskazini na Kwamouth upande wa magharibi wananchi wengi hawakushiriki suala hilo kutokana na sababu za kiusalama.

Baadhi ya wanasiasa wamehoji kuhusu aina ya uchaguzi unaokwenda kufanyika katika nchi hiyo, wakati idadi kubwa ya wananchi wanakabiliwa na tatizo la kiusalama.

Mbali na suala hilo ilibainishwa kuwa tatizo la kuwateuwa wataalamu wa kimataifa kutoka nje ya taifa hilo ambao watapewa jukumu la kukagua daftari la wapigakura, baada ya mashirika ya kiraia na wadau wengine kuhoji kuhudu muda unaotakiwa kikatiba kukamilisha zoezi hilo.



Tayari wanasiasa wa upinzani wakiongozwa na Moise Katumbi na Martin Fayulu wanapinga utaratibu ulioanzishwa na CENI kufanya ukaguzi wa nje wa daftari la uchaguzi.

Kituo cha uchaguzi kinasema kimepokea takriban faili 200 kutoka kwa wagombeaji wa jukumu hilo baada ya Shirika la Kimataifa la La Francophonie (OIF) kukataa jukumu hilo kutokana na muda mfupi wa kumaliza kazi hiyo. **RFI**

# Russia yazidisha mashambulizi Ukraine

**KYIV,** Ukraine

MKUU wa utawala wa kijeshi nchini Ukraine, Sergei Popko, amesema shambulio baya limefanyika mjini Kyiv likihusisha ndege nane kutoka maeneo mbalimbali kwa wakati mmoja, na kwa kutumia, silaha kama makombora ya masafa yaliyoongozwa kulenga eneo hilo.


Kwa mujibu wa mkuu huyo wa kijeshi, shambulio hilo lilifanyika usiku wa kuamkia jana, huku Popko akieleza kuwa shambulio hilo lilikuwa la kipekee kwa ukubwa wake na kwamba lilijumuisha mashambulio ya makombora mengi ya masafa kwa pamoja kwa wakati mfupi.

Pia kwa mujibu wa taarifa za awali mengi kati ya makombora hayo yaliyofyatuliwa yaliangamizwa.

Kwa mujibu wa Meya wa mjini Kyiv, Mayor Klitschko, vipande vya roketi vilianguka katika maeneo tofauti ya mji mkuu katika wilaya za Obolonsky, Shevchenkovsky, Solomensky na Darnitsky- pamoja na hifadhi ya Wanyama ya Kiev.

Popko alisema kuwa uharibifu mkubwa ulionekana katika wilaya ya Solomensky kutokana na moto uliozuka katika makazi yasiyokaliwa na watu na magari kadhaa yaliungua, na kwamba kulikuwa na watu watatu waliouawa katika wilaya ya Solomensky. **BBC**





Waziri wa Mambo ya Ndani wa Somalia, Dk. Mohamed Ali na mwenzake wa Kenya Dk. Kithure Kindiki baada ya kukubaliana kufungua mpaka wao uliofungwa kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# Vita vyazidi kupamba moto Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MAPIGANO makali yameendelea kote katika mji mkuu wa Sudan, Khartoum wakati jeshi likijaribu kulinda kambi zake muhimu ili kutokamatwa na kikosi cha wanamgambo cha msaada wa haraka (RSF).

Inaelezwa kuwa mapigano hayo yameendelea kushuhudiwa jana mjini Khartoum, huku mashambulizi ya angani na ufyatuaji wa mizinga, ikirindima katika mitaa kadhaa ya mji huo.

Mapigano hayo yalianza kutokana na mvutano kuhusu mipango ya RSF kutaka kujiunga na jeshi na kushirikishwa kwenye uongozi wa mpito wa kisiasa wa nchi hiyo kuelekea utawala wa kidemokrasia.

Kwa mujibu wa mashuhuda mashambulizi hayo ya angani yamesikika pia kusini mwa Khartoum, na milipuko mikubwa kutokea kote karibu na Mto Nile ikiwemo miji inayopakana nayo kama Bahri na Omdurman.

Mapigano hayo kati ya jeshi la taifa linaloongozwa na Jenerali Abdel al-Burhan, na kikosi chenye nguvu cha wanamgambo wa Rapid Support (RSF) kinachoongozwa na naibu wa zamani wa mkuu wa majeshi jenerali Mohamed Dagalo, yanafanyika mjini Khartoum lakini yamesababisha pia machafuko katika maeneo mengine ya Sudan hususan jimbo la magharibi Darfur.

Inaelezwa kuwa machafuko hayo yamesababisha mgogoro wa kibinadamu unaotishia kuyumbisha kanda hiyo. Na kwamba tayari zaidi ya watu 700,000 ni wakimbizi wa ndani nchini Sudan na takriban 200,000 wamekimbilia nchi jirani.

Mmoja wa wakazi wa Khartoum Ayman Hassan, alisema hali inazidi kuwa mbaya na kwamba m,ashambulizi yanawafuata kila wanapokwenda hadi mitaani.

"Hatujui kile wananchi walifanya hata wakakabiliwa na vita hadi kwenye makazi yao," alisema.

Inaelezwa kuwa mapambano yameongezeka mjini Khartoum na Geneina, mji mkuu wa jimbo la Darfur Magharibi, tangu pande mbili kwenye mzozo huo zilipoanza mazungumzo ya amani mjini Jeddah Saudi Arabia wiki moja iliyopita, kutokana na ushawishi wa Marekani na Saudia.

Wakazi na mashuhuda walisema wanamgambo wa RSF walishambulia kambi kuu za kijeshi zilizoko kaskazini mwa Omdurman na kusini mwa Khartoum.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa hiyo lilikuwa ni jaribio la kuzuia jeshi kutumia silaha nzito na ndege za kivita, na kwamba limekuwa likijaribu kukatisha njia ambazo wanamgambo wanatumia kupata vifaa kutoka nje ya Khartoum.

Aidha, inaelezwa kuwa jeshi hilo limekuwa likijaribu kulinda maeneo muhimu ya kimkakati ikiwemo uwanja wa ndege ulioko katikati ya Khartoum na kiwanda cha kusafisha mafuta cha Al-Jaili kilichoko Bahri.

Mkuu wa majeshi Jenerali al-Burhan na hasimu wake anayeongoza RSF Jenerali Dagalo maarufu kama Hemedti, walichukua nyadhifa za uongozi kwenye Baraza la kiutawala baada ya mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 2019, yaliyomuondoa aliyekuwa rais wa muda mrefu wa nchi hiyo na aliyetawala kwa mkono wa chuma Omar al-Bashir.

Miaka miwili baadaye majenerali hao walifanya mapinduzi mengine wakati muda wa kukabidhi utawala kwa raia ulipokaribia. Lakini pande zote mbili zilishindwa kuelewana wakati wapatanishi walikuwa wakijaribu kupiga msasa mpango mpya wa mpito.

Aidha, wakati huo huo taarifa zilieleza kwamba Jenerali al-Burhan amemfuta kazi kaimu waziri wa mambo ya ndani, Anan Hamed Omar, ambaye pia ni mkuu wa polisi.

Taarifa zinasema Jenerali Burhan, alimtaja Khalid al-Din kama mkurugenzi mkuu mpya wa polisi, huku ikielezwa kuwa hakukuwa na sababu yoyote iliyotolewa juu ya waziri huyo kufutwa kazi, ikiwa ni muendelezo kwani awali gavana wa benki kuu na mawaziri wawili wa kigeni nao waliondolewa katika nmafasi zao.

Inabainishwa kuwa Polisi imekuwa haifanyi kazi katika maeneo yaliyokumbwa na machafuko, ikiwa ni pamoja na mji mkuu wa Khartoum, tangu mapigano yalipoanza Aprili 15. Na kwamba imeshababisha kushamiri kwa vitendo vya ukikaji wa sheria, ukiwemo uporaji na wizi. **DW/BBC**

# ZAHERA NA HESABU ZA VIDOLE AKIZIWINDA AZAM FC, SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, ni kama anapigia hesabu za 'vidole' wakati huu akisaka pointi sita katika michezo miwili iliyosalia ili kufanikisha malengo ya kuendelea kusalia katika mikikimikiki ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu ujao.

Baada ya juzi kufanikiwa kuvuna pointi tatu dhidi ya Mtibwa Sugar, sasa Polisi Tanzania wanahitaji alama tatu dhidi ya Simba ambao watakutana nao Mei 24 na 28 watamaliza msimi na Azam FC mechi zinazotarajiwa kupigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

**Polisi Tanzania iko nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na pointi 25 na wakifanikiwa kupata alama zote sita katika mechi hizo mbili watakuwa na jumla ya alama 31, ambazo zinaweza kuwatoa kwenye nafasi hiyo kutegemeana tu na kama Mbeya City yenye alama 30, KMC FC pointi 29 sawa na Mtibwa Sugar, zitapoteza mechi zao mbili za mwisho.**

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera alisema wamejipanga vizuri kuelekea michezo miwili iliyosalia kuhakikisha wanapata pointi sita ili kuinusuru timu hiyo kuendelea kubaki katika ligi hiyo.

Alisema ushindi walioupata katika mechi iliyopita umesaidia wachezaji wake kujiamini na kuendelea kupambana katika mechi mbili zilizosalia kuhakikisha wasaka pointi zote sita ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuepuka kucheza Championship msimu ujao.

"Hatuko kwenye nafasi nzuri kwenye msimamo, tunatakiwa kupambana kushinda mechi zote zilizosalia kujiweka kwenye nafasi nzuri za kuendelea kusalia Ligi Kuu msimu ujao,"alisema Zahera.

Aliongeza kuwa michezo iliyosalia ni migumu kwa sababu watakuwa ugenini na wachezaji wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanafanikiwa kupata alama zote sita.

"Mechi zote mbili tutacheza ugenini, tunakutana na timu ambazo zinahitaji kupata matokeo, lakini na sisi tunahitaji ushindi katika michezo yote hiyo kwa sababu ya hali yetu katika msimamo," alisema kocha huyo.

## Mayele, Sakho wampa mzuka Sheva Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WINGA na mshambuliaji wa zamani wa Simba, Miraji Athumani 'Sheva', ameelezea furaha yake ya kurejea tena Ligi Kuu akiwa na timu yake mpya ya JKT Tanzania, kwa kuwa alikuwa akitamani kucheza ligi moja na straika wa Yanga, Fiston Mayele na winga wa Simba, Pape Sakho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Miraji ambaye aliichezea Klabu ya Simba mwaka 2019 hadi 2020, alisema ni bahati iliyoje kurejea tena kwenye Ligi Kuu na kwamba ndoto yake ilikuwa kuwa ligi moja na baadhi ya mastaa anaowakubali kwa sasa, Mayele na Sakho.

"Nawakubali wengi, lakini hawa wachezaji wanacheza kwenye nafasi ambayo mimi nacheza na naiga vitu vingi kutoka kwao, mimi ni straika na winga pia, Mayele yeye kosa moja goli moja, Sakho ni msumbufu, mimi pia kuna viti naokota huko, sasa na mimi nimekuja huko huko, nitaonyesha nilichokuwa nacho, kikubwa tu ni kumuomba Mungu nisipate majeraha," alisema Miraji ambaye mashabiki wake wanamwita 'Sheva', wakimfananisha na straika wa zamani wa Chelsea, AC Milan na timu mbalimbali za barani Ulaya, Andriy Shevchenko.

Akiwa ni mmoja wa wachezaji walioipandisha daraja JKT Tanzania kutoka Ligi ya Championship msimu huu, amethibitisha kubaki kwenye kikosi hicho kwa sababu hajapokea ofa yoyote kutoka timu zingine.

"Safari ya Championship ilikuwa ndefu na ngumu, nilimisi kucheza Ligi Kuu na timu kubwa, timu nzuri ili nionyeshe tena nilichokuwa nacho kwa sababu mashabiki wengi hawajaniona na wamenisahau kwani muda mrefu sikucheza soka kutokana na kuwa majeruhi.

"Nilipata majeraha, nilivunjika mfupa mdogo wa mguu wa kushoto, ndicho kilichosababisha kupotea kwa muda mrefu kwenye ramani ya soka, sasa nimepona, maisha yanaendelea nipo JKT Tanzania si Simba tena," alisema.

**WANIA...**



Wachezaji wa timu ya mpira wa Kikapu ya Vijana wanaolelewa katika Kituo cha JMK Park, wakifanya mazoezi kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUNMANNE JUMA**

## Twanga Pepeta sasa wapeleka kilio chao NEMC

**Na Sabato Kasika**

SIKU chache baada ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kufungia kumbi za starehe kwenye baadhi ya maeneo nchini kwa kukiuka kanuni na sheria za uhifadhi wa mazingira, Bendi ya Twanga Pepeta imeliomba kuangalia upya uamuzi huo.

Meneja wa bendi hiyo, Hassan Rehani, amesema Twanga Pepeta ilikuwa na maonyesho sita, lakini sasa wamiliki wa kumbi wanaogopa faini na kufungiwa na baraza hilo.

"Kauli za Mkurugenzi Mkuu wa NEMC zinanishangaza, mara nyingi waathirika ni wanaopigiwa kelele na sisi. Sijengi uhalali kwamba tunachokifanya sisi ni halali, lakini NEMC inapaswa kukaa katikati itusaidie na wale wanaopata usingizi," amesema Rehan.

Rehani (pichani) ameelezea hayo kupitia mtandao wa kijamii na kuongeza kuwa habari ya vipimo sauti bado wana mashaka navyo, kwamba watu wanapigwa faini, lakini vipimo hivyo vya sauti hata baadhi ya maofisa wa NEMC hawajui jiografia ya eneo husika.

"NEMC watueleze wanaanza kupima wapi au wanapimaje. Watusaidie wasanii wapate haki zao na wale wanaokosa usingizi wapate haki zao, si kuegemea upande mmoja," alisema.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baada ya kutafakari athari za kiuchumi, wafanyabiashara 20 walioandika barua na kukiri makosa yao walifunguliwa kumbi zao.

Mei 8, mwaka huu, NEMC ilizifungia baa na kumbi za starehe 89 za majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma baada ya kubaini kupiga kelele na mitetemo iliyozidi viwango vinavyotakiwa.



Mara ya kwanza baraza hilo lililazimika kuwafungia baada ya kutoa elimu kwa miaka mitano, ambapo mkurugenzi huyo alisema watu walikuwa hawalali, huku malalamiko yakiongezeka.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA ATAKIWA PSG

NYOTA wa Manchester City, Bernardo Silva, anasakwa zaidi na Paris St-Germain wanaotaka kumchukua kiungo huyo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 28, kuchukua nafasi ya mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, 35. ***(Le Parisien)***

### RICE ANYATIWA ARSENAL

ARSENAL ipo tayari kuipa West Ham kiasi cha pauni milioni 90 ambayo ni rekodi ya klabu kwa ajili ya kiungo wa kati wa England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24, wakati Granit Xhaka wa Uswisi (30), anaweza kuwa mmoja wa wachezaji watakaouzwa na 'Washikabunduki' hao. ***(Mail)***

### ALLISTER AITAKA UEFA

KIUNGO wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool na Manchester United, anataka kujiunga na klabu inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ataondoka Brighton msimu huu wa majira ya joto. ***(Athletic)***

### POCHETTINO NA MOUNT

KOCHA mpya mtarajiwa wa Chelsea, Mauricio Pochettino, anatazamiwa kufanya mazungumzo na Mason Mount ili kumshawishi kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24, kuongeza mkataba wake ambao unamalizika msimu wa majira ya joto wa 2024. ***(Football Insider)***

### NEVES AWANIWA BARCA

KIUNGO wa kati wa Wolves, Ruben Neves, 26, anasakwa na Barcelona, huku klabu yake hiyo kutoka Midlands ikitaka angalau pauni milioni 45 ili wamruhusu mchezaji huyo kuondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imeongeza kasi ya kumnasa kiungo wa Hungary, Dominik Szoboszlai, 22, ambaye ana kipengele cha kuuzwa kwa euro milini 70 katika mkataba wake na RB Leipzig, lakini hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanyika kati ya klabu hizo. ***(Sky Sports)***

### AIVUTIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United pia inavutiwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallaghe, 23. ***(Mail)***

### ALVAREZ ATAJWA BAYERN

KLABU za Bayern Munich na Borussia Dortmund zote zinamtaka kiungo wa kati wa Mexico, Edson Alvarez, 25, ambaye Ajax inaweza kuwa tayari kumuuza kwa pauni milioni 30. ***(SPORT1)***

### JONES, TUANZEBE KUUZWA

WALINZI wa England, Phil Jones, 31 na Axel Tuanzebe (25), wanatarajiwa kuuzwa na Manchester United msimu huu wa majira ya joto. ***(ManchesterEveningNews)***

### KOBEL KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Borussia Dortmund, Gregor Kobel, ingawa klabu hiyo ya Ujerumani inakusudia kumpa mkataba mpya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uswizi mwenye umri wa miaka 25. ***(Independent)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: LIVER ITAPIGANIA NNE BORA HADI MWISHO

**LIVERPOOL,** England

**Amesema wiki sita au saba zilizopita hakuamini inaweza kutokea na kwamba sasa...**

KOCHA Jurgen Klopp amesema Liverpool haitaacha kupigania nafasi ya nne bora na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Leicester juzi, Jumatatu.

**Mabao mazuri ya Curtis Jones na Trent Alexander-Arnold yaliweka msukumo wao kwa timu nne bora huku yakiwatupa 'Mbweha' hao karibu na kushuka daraja.**

Leicester walio nafasi ya pili kutoka chini wamo pointi mbili kutoka kwenye usalama wa kubaki Ligi Kuu zikiwa zimesalia mechi mbili na wanakwenda Newcastle United Jumatatu ijayo.

Ushindi huo unamaanisha kuwa Liverpool wamekata tiketi ya kucheza Ligi ya Europa msimu ujao na wanashika nafasi ya tano, pointi moja nyuma ya Newcastle na Manchester United, ambazo zote zimecheza mechi pungufu.

Klopp alisema: "Kazi yetu ni kuweka presha (kwa Newcastle na Manchester United), lakini kama sivyo hii tayari ni bora kuliko tulivyotarajia wiki sita au saba zilizopita.

"Sijui inamaanisha nini kwetu. Miaka minne au mitano iliyopita tulikuwa na Chelsea shingoni na walikuwa wakishinda kila wakati. Nadhani ulikuwa mwaka tuliomaliza wa nne na ilibidi twende katika mchujo.

"Tulilazimika kushinda kushinda, kushinda, kushinda, kwa sababu wa nyuma yetu walikuwa wakishinda kila wakati huo.

"Tulifanikiwa. Lakini inakuweka kwenye vidole vyako na hiyo ni kazi yetu - tunapaswa kuwaweka kwenye vidole vyao na kisha tutaona kitakachotokea.

"Wiki sita au saba zilizopita sikuamini inaweza kutokea. Tulichokosa wakati huo ni uthabiti.

"Mchezo haujawahi kuwa ambao ungeweza kuwa, pambano la kweli, changamoto kila mahali, kwa sababu tuliudhibiti kwa njia ya kushawishi."

Alisson Becker alimnyima nafasi ya mapema Jamie Vardy na Liverpool wakachukua udhibiti haraka, huku Jones akifunga mara mbili.

Kiungo huyo alifungua ukurasa wa mabao baada ya dakika 33 akiunganisha krosi ya Mohamed Salah.

Dakika tatu baadaye alitumia tena vizuri pasi nyingine ya Salah kuzunguka na kumpita Daniel Iversen kutoka ndani ya boksi na kufunga bao.

Harvey Barnes alimjaribu Alisson mapema katika kipindi cha pili, lakini kulikuwa na pambano kidogo kutoka kwa 'Mbweha' na Liverpool hatimaye kurahisisha ushindi.

Alexander-Arnold alifunga pointi kwa shuti kali la umbali wa yadi 25 kutokana na Salah kupiga shuti fupi la faulo zikiwa zimesalia dakika 19 tu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,114,9

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 17,18 NA 19 MEI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/05/23 | 19:00 | Marumo Gallants FC vs Young Africans | 2.50 | 3.30 | 2.50 |
| 02. 17/05/23 | 19:00 | AEL Limassol vs Karmiotissa | 2.69 | 3.27 | 2.48 |
| 03. 17/05/23 | 19:30 | IF Karlstad Fotboll vs Hammarby Talang FF | 2.29 | 3.59 | 2.53 |
| 04. 17/05/23 | 20:00 | Ankaragucu vs Antalyaspor | 2.28 | 3.41 | 2.83 |
| 05. 17/05/23 | 21:30 | National Bank vs Ismaily SC | 2.39 | 2.95 | 3.05 |
| 06. 17/05/23 | 21:35 | Airdrieonians vs Hamilton | 2.45 | 3.23 | 2.66 |
| 07. 18/05/23 | 02:00 | Sport Recife vs Sao Paulo | 2.80 | 2.96 | 2.47 |
| 08. 18/05/23 | 02:30 | Toronto FC vs NY Red Bulls | 2.37 | 3.26 | 2.94 |
| 09. 18/05/23 | 03:30 | America Mineiro MG vs Internacional | 2.56 | 3.01 | 2.65 |
| 10. 18/05/23 | 22:00 | AZ Alkmaar vs West Ham | 2.68 | 3.24 | 2.51 |
| 11. 18/05/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Juventus | 2.35 | 3.14 | 2.98 |
| 12. 19/05/23 | 03:00 | Arsenal Sarandi vs Independiente | 2.90 | 2.85 | 2.47 |
| 13. 19/05/23 | 19:00 | Hillerod vs HB Koge | 2.44 | 3.13 | 2.62 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SABITZER AONDOLEWA UNITED



**MANCHESTER,** England

MARCEL Sabitzer ameondolewa kwenye mechi tatu za mwisho za Manchester United msimu huu wa Ligi Kuu England na pia kwenye fainali ya Kombe la FA mwezi ujao kwa sababu ya jeraha la goti.

Mchezaji huyo wa Austria mwenye umri wa miaka 29, ambaye alijiunga na United kwa mkopo kutoka Bayern Munich Januari, alikosekana kwenye ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolves Jumamosi na vipimo vimefichua tatizo la goti na hivyo kumaliza msimu wake mapema.

Taarifa ya Man United imesema; “Kila mmoja katika klabu amesikitishwa na kupoteza huduma ya Marcel, huku tukiwa tunatafuta kumaliza msimu kwa nguvu kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA, na tunashukuru kwa mchango wake katika maendeleo yetu hadi sasa.”

Sabitzer aliletwa siku ya mwisho kwa sababu ya majeraha ya viungo wenzake, Christian Eriksen na Scott McTominay na amefunga mabao matatu katika mechi 18 alizocheza katika klabu hiyo ya Old Trafford.

Aliimarisha matumaini ya United ya kucheza fainali baada ya kufunga bao katika ushindi wa penalti wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Brighton ambapo sasa watacheza na Manchester City, Juni 3, mwaka huu.

Sabitzer aliingia kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa United dhidi ya Newcastle United katika fainali ya Kombe la Carabao Februari mwaka huu.



## *City yakomaa kumbakiza Gundogan*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City haijakata tamaa ya kukubaliana mkataba mpya na Ilkay Gundogan na haijafahamishwa kuwa ana nia ya kuondoka msimu huu wa majira ya joto, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mkataba wa Gundogan unatarajiwa kuisha Juni na iwapo masharti mapya hayatakubaliwa, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani ataondoka Etihad kwa uhamisho huru.

Hali ya mkataba wake imewatahadharisha Barcelona na angalau klabu moja nchini Italia, lakini City pia wangependa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, abaki angalau kwa msimu mwingine.

City wana nia ya kumbakisha nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, kwa sehemu kwa sababu ya mashaka kuhusu viungo wengine katika kikosi cha Pep Guardiola.

Kalvin Phillips amepata shida kupata nafasi kutokana na kuhama kwake kutoka Leeds United msimu uliopita wa majira ya joto, wakati vyanzo viliiambia ESPN kwamba Bernardo Silva yuko tayari kuondoka ikiwa ofa inayofaa itawasili kutoka kwa klabu n ingine kubwa Ulaya.

City hawafichi nia yao y kumnunua Jude Bellinghar lakini hawajawasilisha o kwa wawakilishi wa kinc huyo mwenye umri wa mial 19, au kwa Dortmund na kur hisia kwamba Real Madr wako mbele katika mbio z kuwania saini yake.

Gundogan amekuw muhimu kwa City msimu hu akifunga mabao yote maw katika ushindi wa 2-1 dhi ya Leeds United na kufung mawili katika ushindi wa 3 dhidi ya Everton Jumapili.

HABARI MICHEZO


65,687/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/05/23 | 17:00 | Fulham FC vs Crystal Palace | 2.33 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 20/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Everton FC | 2.55 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 20/05/23 | 17:30 | FC Arouca vs GD Chaves | 2.44 | 3.25 | 2.70 |
| 04. 20/05/23 | 18:00 | FC Nantes vs Montpellier HSC | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 05. 20/05/23 | 19:15 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.27 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 20/05/23 | 22:00 | Lille OSC vs Olympique Marseille | 2.25 | 3.45 | 2.80 |
| 07. 21/05/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Fluminense FC RJ | 2.65 | 3.30 | 2.44 |
| 08. 21/05/23 | 00:30 | America FC MG vs Fortaleza EC CE | 2.45 | 3.40 | 2.60 |
| 09. 21/05/23 | 14:30 | Club Brugge vs Royal Antwerp FC | 2.23 | 3.20 | 2.65 |
| 10. 21/05/23 | 15:30 | SK Rapid Wien vs LASK | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 21/05/23 | 15:30 | West Ham United vs Leeds United | 2.22 | 3.35 | 2.95 |
| 12. 21/05/23 | 16:30 | FSV Mainz vs VfB Stuttgart | 2.35 | 3.40 | 2.70 |
| 13. 21/05/23 | 19:00 | SSC Napoli vs Inter Milano | 2.90 | 3.25 | 2.28 |
| 14. 21/05/23 | 19:00 | Adana Demirspor vs Besiktas Istanbul | 2.48 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 21/05/23 | 19:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.17 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 21/05/23 | 21:30 | CA Belgrano vs CA Talleres de Cordoba | 2.95 | 2.85 | 2.22 |
| 17. 21/05/23 | 22:30 | Sporting Lisbon vs Benfica Lisbon | 2.48 | 3.45 | 2.50 |

MECHI ZA USHINDI
“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE
“2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 17/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3206 | Tochigi SC vs Tokyo Verdy | 3.64 | 2.97 | 2.01 |
| 13:00 | 4953 | JEF United Chiba vs Shimizu S Pulse | 3.54 | 3.29 | 1.91 |
| 13:00 | 5170 | Roasso Kumamoto vs Vegalta Sendai | 2.61 | 3.17 | 2.43 |
| 13:00 | 5318 | Fujieda MYFC vs Jubilo Iwata | 3.29 | 3.50 | 1.92 |
| 13:00 | 5997 | Tokushima Vortis vs Zwiegen Kanazawa | 2.11 | 3.25 | 3.04 |
| 14:00 | 4294 | Astana vs FK Turan | 1.24 | 5.10 | 10.40 |
| 15:00 | 2625 | Lernayin Artsakh vs Urartu | 12.43 | 5.80 | 1.18 |
| 15:00 | 4015 | Saint George FC vs Hawassa Kenema SC | 1.74 | 3.37 | 4.36 |
| 16:00 | 5968 | Kairat Almaty vs Atyrau | 2.00 | 3.05 | 3.68 |
| 17:00 | 4479 | Basaksehir vs Umraniyespor | 1.70 | 3.72 | 4.40 |
| 17:00 | 4805 | Vojvodina vs Cukaricki St | 2.41 | 3.05 | 2.79 |
| 17:00 | 5167 | FK Tukums 2000/Tss vs Valmiera Fk/Bjss | 7.43 | 4.95 | 1.31 |
| 17:30 | 1280 | Khalijfars Mahshahr vs Chooka Talesh FC | 2.19 | 2.89 | 3.36 |
| 17:30 | 1832 | Shahrdari Hamedan vs Saipa Karadj | 3.05 | 2.59 | 2.59 |
| 17:30 | 2781 | Caspian Babol vs Mes Shahr-e Babak | 2.27 | 2.55 | 3.30 |
| 17:30 | 3049 | Fajr Sepasi vs Pars Jonoubi Jam | 1.85 | 2.99 | 4.44 |
| 17:30 | 3184 | Arman Gohar Sirjan vs Shams Azar Qazvin | 5.61 | 3.63 | 1.55 |
| 17:30 | 3411 | Khosheh Talaei vs Esteghlal Khuzestan | 3.21 | 2.69 | 2.39 |
| 17:30 | 4876 | Shahrdari Astara vs Kheybar Khorramabad FC | 3.94 | 2.70 | 2.10 |
| 18:00 | 2445 | Sidama Bunna SC vs Mekelakeya | 2.75 | 2.80 | 2.64 |
| 18:00 | 3190 | FK Liepaja vs Rigas Futbola Skola | 5.19 | 3.89 | 1.54 |
| 18:00 | 4430 | Ordabasy vs FK Kyzylzhar Petropavlovsk | 2.08 | 2.95 | 3.57 |
| 18:00 | 4697 | CS Constantine vs JS Saoura | 1.79 | 3.27 | 4.26 |
| 18:35 | 2085 | Al Ain vs Al Nasr Dubai | 1.39 | 4.20 | 5.60 |
| 19:00 | 3345 | Marumo Gallants FC vs Young Africans | 2.50 | 3.30 | 2.50 |
| 19:00 | 2091 | FC Honka/Akatemia vs FC Ilves-Kissat | 1.30 | 5.60 | 6.64 |
| 19:00 | 2245 | Zrinjski Mostar vs Velez Mostar | 1.61 | 3.57 | 5.07 |
| 19:00 | 3121 | Shirak Gyumri vs Ararat Armenia | 5.99 | 3.98 | 1.47 |
| 19:00 | 4223 | AEL Limassol vs Karmiotissa | 2.33 | 3.21 | 2.95 |
| 19:25 | 2007 | AL Hazm vs AL Sahel SC | 1.29 | 4.40 | 7.20 |
| 19:25 | 4708 | AL Arabi (SA) vs AL Ain | 2.06 | 2.95 | 3.20 |
| 19:30 | 2610 | IF Karlstad Fotboll vs Hammarby Talang FF | 2.31 | 3.49 | 2.56 |
| 19:30 | 2977 | FC Krasnodar vs Ural Yekaterinburg | 1.85 | 3.42 | 3.73 |
| 19:30 | 5890 | Backa Topola vs Red Star Belgrade | 5.17 | 3.88 | 1.54 |
| 20:00 | 1964 | Falkenbergs vs Tvaakers IF | 1.36 | 4.21 | 7.18 |
| 20:00 | 2160 | Fatih Karagumruk vs Adana Demirspor | 2.99 | 3.83 | 2.04 |
| 20:00 | 3270 | Ljungskille vs Vanersborgs IF | 1.92 | 3.24 | 3.55 |
| 20:00 | 3771 | Torns IF vs Lunds BK | 3.34 | 3.24 | 1.99 |
| 20:00 | 4547 | Ankaragucu vs Antalyaspor | 2.30 | 3.36 | 2.84 |
| 20:00 | 4769 | Ariana FC vs BK Olympic | 2.05 | 3.19 | 3.24 |
| 20:00 | 5704 | Dalkurd FF vs IFK Stocksund | 1.44 | 4.12 | 5.77 |
| 20:00 | 5876 | Sandvikens IF vs Taby FK | 1.65 | 3.84 | 4.10 |
| 20:00 | 5980 | Norrby IF vs FC Trollhattan | 3.55 | 3.24 | 1.92 |
| 20:20 | 3646 | Alshoulla vs Al Ahli Jeddah | 6.37 | 4.11 | 1.41 |
| 20:30 | 3071 | Vasalunds IF vs United IK Nordic | 1.89 | 3.55 | 3.34 |
| 21:30 | 3871 | National Bank vs Ismaily SC | 2.45 | 2.91 | 3.01 |
| 21:35 | 2532 | Airdrieonians vs Hamilton | 2.02 | 3.44 | 3.23 |
| 22:00 | 1290 | USM Alger vs ASEC Mimosas | 1.94 | 3.24 | 3.49 |
| 22:00 | 4717 | Manchester City vs Real Madrid | 1.63 | 3.89 | 4.55 |
| 22:00 | 5088 | Middlesbrough vs Coventry | 1.82 | 3.39 | 4.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# BINGWA LIGI KUU WANAWAKE BARA KUTANGAZWA IRINGA LEO

Na Adam Fungamwango

LIGI Kuu ya Soka la Wanawake Tanzania Bara msimu wa 2022/23, inatamatika leo kwenye viwanja mbalimbali, huku bingwa akipewa nafasi kubwa ya kutangazwa akiwa mkoani Iringa.

**Maafande wa JKT Queens ndiyo kwa kiasi kikubwa wanatabiriwa kutwaa ubingwa kutokana na kucheza mechi yao dhidi ya timu dhaifu inayoshika mkia, Mkwawa Queens, mechi itakayofanyika Uwanja wa Samora, Iringa.**

Mabingwa wa ligi hiyo kwa misimu mitatu mfululizo, Simba Queens, nao watakuwa huko huko Iringa kucheza dhidi ya Ceasiaa Queens, mechi ikipigwa Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa.

Kwa maana hiyo timu hizo mbili, JKT Queens na Simba Queens, ambazo zipo katika nafasi ya juu zikichuana kutwaa ubingwa msimu huu, zote zitakuwa mkoani humo, hivyo msimu huu bingwa atajulikana akiwa Iringa.

JKT Queens inaongoza kwa kuwa na pointi 43, hivyo ikishinda itafikisha pointi 46 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote.

Simba Queens inachoombea ni maafande hao wafungwe au kutoka sare na wao kushinda, kitu ambacho ni kigumu kutokana na ubora wa JKT Queens na udhaifu wa timu inayocheza nayo ambayo inaburuza mkia ikiwa na pointi tatu tu.

Ili Simba Queens iwe bingwa, inapaswa JKT Queens ifungwe au kutoka sare na yenyewe iibuke na ushindi dhidi ya Ceasiaa Queens, vinginevyo hata ikishinda itafikisha pointi 45 ambazo maafande watakuwa wamezipita wakishinda mechi ya mwisho.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, pamoja na kukubali lolote litakalotokea, ameshauri kuwapo na michuano mingine kama Kombe la FA ili kuwapa nafasi wachezaji wa kike kucheza mechi nyingi tofauti na sasa ambapo ligi ina timu 10 tu, zikichezwa mechi 18 pekee.

“Ligi ya Tanzania ni ngumu na nzuri, imekusanya wachezaji wazuri wa ndani na nje, ninachoshauri ni kuongezwa kwa timu kidogo kwenye ligi hii, pia kuwe na michuano mingine kama ya Kombe la FA, ili hawa watoto wa kike wawe na muda mrefu wa kucheza,” alisema.

Ligi hiyo inatamatika leo kwa mechi zingine kuchezwa Uwanja wa Nyamagana, Mwanza, baina ya Alliance Queens na Baobab Queens, Fountain Gate Princess dhidi ya The Tigers Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, na katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi, Amani Queens itaikaribisha Yanga Princess.

SOKA...



Baadhi ya vijana kutoka maeneo mbalimbali wakifanya mazoezi katika Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete (JMK Park), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga yapania historia Sauzi leo*

INATOKA UKURASA 24

na Khanyisa Mayo wa Cape Town City.

“Ni kweli uongozi moja ya malengo yake ni kuona unafanikiwa kupata mshambuliaji mmoja mkubwa kutoka hapa Afrika Kusini kwa ajili ya msimu ujao. Hata rais Injinia Hersi Said, ameshatoa muongozo na mipango yake kuwa yupo kwenye jitihada hizo kuona Yanga inafanikiwa kushusha mshambuliaji kutoka Afrika Kusini na ameeleza kwenye mahojiano yake na mwandishi nguli wa Afrika Kusini, Robert Marawa, “ alisema mtoa taarifa huyo.

Alipotafutwa Mkuu wa Idara ya Habari ya Yanga, Ali Kamwe, alikiri kuwapo kwa mpango huo huku akishindwa kuweka wazi ni mshambuliaji kutoka timu gani kati ya wanaowawania.

“Ni kweli huo mpango upo, lakini ninachoweza kusema ni wale ambao wanapambana katika orodha ya wafungaji wakiwa na mabao sawa japo kuwa kwa sasa mipango yetu ipo kwanza kwenye mchezo wa kesho (leo),” alisema Kamwe.

# Michezo

Jumatano Mei 17, 2023
Nipashe



Sabitzer aondolewa United UKURASA 22

# YANGA SC YAPANIA HISTORIA SAUZI LEO

## ●●● Nabi aanika mkakati mzito kuimaliza Marumo CAF, uongozi nao wageukia...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA wapya wa soka Tanzania, Yanga, leo wanaweza kuingia kwenye rekodi ya kuingia fainali ya Kombe la Shirikisho la Afrika kwa mara ya kwanza, kama wataweza kulinda ushindi wao wa mabao 2-0 waliyoyapata nchini, Mei 10, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakihitaji sare au kufungwa bao lisilozidi moja, itaporudiana dhidi ya Marumo Gallants nchini Afrika Kusini.

Yanga itashuka kwenye Uwanja wa Royal Bafokeng nchini Afrika Kusini, saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki kucheza mechi hiyo ya mkondo wa pili ya hatua ya nusu fainali ambayo itaamua hatma ya timu zote mbili, huku ikipania kuweka rekodi iliyowekwa mwaka 1993 na Simba ambayo ilifanya hivyo wakati huo likiitwa Kombe la CAF kwa kuifunga Atletico Sport Aviacao ya Angola jumla ya mabao 3-1, iliyoshinda kwenye mechi ya kwanza Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru) na kwenda kusuluhu ugenini.

**Pia, Yanga itakuwa imeweka rekodi ya kutinga fainali kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo iliyoanzishwa mwaka 1935 jijini Dar es Salaam.**

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema amekiweka tayari kikosi chake kwa ajili ya mechi hiyo ngumu, huku akili yake kubwa ikiwa ni kulinda kile ambacho imekipata nchini kwenye mechi ya kwanza.

Alisema kwa jinsi aliivyoitazama Marumo Gallants si timu ya kubeza na kwa sababu tayari wameshapata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani, kikubwa kwao atakachofanya ni kuulinda kwa gharama yoyote, ikiwa ni pamoja na kuwashtukiza wageni kwa bao la ugenini ambalo anadhani litawachanganya na kuifanya mechi kuwa ngumu kwa Wasauzi hao.

"Mechi haitokuwa rahisi kwa sababu wapinzani wetu wana timu nzuri, lakini wana mapungufu yao pia ambayo kama tutayatumia vema tunaweza kufanikiwa katika hili. Wana safu nzuri sana mbele sehemu ya ushambuliaji, hivyo mabeki nimewataka kuwa makini sana, lakini wana shida sehemu ya ulinzi na huo ndiyo mtaji wetu mkubwa kuelekea kwenye mechi hii kwani tunahitaji kuwashtukiza kwa kupata bao moja ili kuvuruga mipango yao yote," alisema Mtunisia huyo.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo umesema umepanga kufanya usajili mzito wa kung'oa mmoja kati ya washambuliaji hatari kwenye Ligi Kuu ya Afrika Kusini kwa ajili ya kufanya vizuri zaidi kimataifa na Ligi Kuu msimu ujao.

Taarifa zilizolifikia Nipashe jana kutoka kwa mmoja wa viongozi wa timu hiyo, zimeeleza licha ya kuwa na mchezo mgumu wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho, pia wanapambana kuhakikisha wananasa mmoja kati ya washambuliaji hatari katika ligi ya nchi hiyo.

Katika ligi ya Afrika Kusini washambuliaji hatari zaidi ni Mnamibia Peter Shalulile wa Mamelod Sundowns mwenye mabao 12 sawa

INAENDELEA UKURASA 23

**TUTAWASHIKA TENA...**



Viungo wa Yanga, Mudathir Yahya (mbele) na Khalid Aucho, wakiwa katika utani wakati wa mazoezi ya timu hiyo Afrika Kusini jana kujiandaa na nusu fainali ya mkondo wa pili ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants FC ya nchini humo itakayopigwa leo katika Uwanja wa Royal Bafokeng uliopo Rustenburg, Sauzi. Kushoto ni kocha wa viungo wa timu hiyo. **PICHA: YANGA**

## Mayele na Sakho wamtia ari Sheva

**Na Adam Fungamwango**

WINGA na mshambuliaji wa zamani wa Simba, Miraji Athumani 'Sheva', ameelezea furaha yake ya kurejea tena Ligi Kuu akiwa na timu yake mpya ya JKT Tanzania, kwa kuwa...



HABARI UKURASA. 20



## Bingwa Wanawake kutangaziwa Iringa

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu ya Soka Wanawake Tanzania Bara msimu wa 2022/23, inatamatika...

HABARI UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >